# Nipashe

Jumatano Februari 28, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581600

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

Maoni@guardian.co.tz

www.facebo...etz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**KONDAKTA** auawa kisa kudai nauli mpya ya daladala

UKURASA 3



**ZIARA YA KUSHTUKIZA** Kampuni matatani kutolipa mishahara wafanyakazi wake

UKURASA 7



**BEI YA SUKARI** yampeleka selo mfanyabiashara

UKURASA 3

# FUNGA KAZI

LICHA ya mvua kubwa, CHADEMA waandamana; Lissu aibua mapya bei ya sukari, Mbowe adokeza Azimio la Mtwara.... Uk. 2




Wanachama na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Freeman Mbowe (aliyenyoosha mkono juu), wakishiriki maandamano ya amani katika barabara kuu ya Arusha-Moshi, jijini humo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Waumini wa kanisa wafungwa jela kwa kuzuia watoto kupata chanjo

UKURASA 5

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Pindi Chana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, wakiongoza waombolezaji katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jana, kutoa heshima za mwisho kwa miili ya watu waliofariki dunia kwenye ajali iliyotokea Februari 24 mwaka huu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### ILIVYOAGWA MIILI YA WATU 25 WALIOFARIKI AJALI YA ARUSHA

VILIO vilitanda wakati miili ya watu 11 kati ya 25 waliofariki dunia katika ajali iliyohusisha magari manne jijini Arusha mwishoni mwa wiki, ilipowasili jana kwenye Uwanja wa Shekhe Amri Abeid kwa ajili ya kuagwa.

Miongoni mwa waliofariki katika ajali hiyo iliyotokea...

UKURASA WA 24

### GAMONDI: HAIJAISHA MPAKA AL AHLY AKAE

LICHA ya timu yake kukata tiketi ya kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku ikiwa na mechi moja mkononi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hawezi kusema ameridhika kwa kuwa kazi haijaisha hadi...



## Bibi kizimbani kwa mashtaka kuchoma moto makalio wajukuu

UKURASA 5

**HABARI** **PM ABAINI KIGOGO KUPIGA MIL. 213/-** UK. 4

**KATUNI** UK. 6

# Fungakazi maandamano CHADEMA

Na Waandishi Wetu, ARUSHA

NI fungakazi maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na maandamano ya chama hicho yaliyofanyika jijini jana huku yakikusanya mamia ya watu kutoka pande zote za jiji na mikoa ya jirani ya Kanda ya Kaskazini.

Licha ya jiji la Arusha kusimama kwa zaidi ya saa moja kutokana na mvua kubwa iliyonyesha ikiambatana na upepo, mamia ya waandamanaji na viongozi wa CHADEMA hawakuondoka barabarani kusubiri ipite.

Badala yake, waliendelea na maandamano huku viongozi wake wakisema wananchi wa Arusha ili kwa siku moja kula wali nyama, unahitaji kuwa na kati ya Sh. 20,000 na 22,000.

Wakati wote wa maandamano, katika njia nne zilizokuwa zimeandaliwa, wimbo mahususi wa hamasa uliotumika kuwavutia vijana wa Arusha, ulikuwa ukipigwa. Wimbo huo ni 'One Love' wa mwanamuzi maarufu wa Reggae duniani na raia wa Jamaica, Robert Nester Marley (Bob Marlery).

Hata hivyo, kundi la waandamanaji lililoanzia eneo la JR Mbauda kupitia Ngarenaro, Kona ya Nairobi hadi Relini, lilikumbana na adha ya msongamano wa magari baada ya polisi kuamuru waandamaji kutembea upande mmoja ili kupisha shughuli zingine za barabara.

Uwanja wa Relini ulifurika zaidi kuanzia saa 8:40 mchana baada ya waandamanaji waliokuwa wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu, kutokea Mbauda kuwasili.

Baadaye, mamia ya wafuasi na wanachama wa CHADEMA waliongeza hamasa saa 8:50 mchana baada ya Mwenyekiti wa Taifa wa chama, Freeman Mbowe, kuingia uwanjani hapo akitokea kundi la waandamanaji walioanzia Kwa Mrefu kupitia Ngulelo, Mianzini, Barabara ya Makongoro, Barabara ya Sokoine, Meru, Fire, Soko la Samunge hadi uwanjani hapo.

Dk. Willibrod Slaa, Katibu Mkuu wa zamani wa CHADEMA, aliwasili saa 8:55 na waandamanaji akitokea Makao Makuu ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kuelekea JR Mbauda, ambako waliungana na Lissu.

**KAULI YA LEMA**

Baada ya kuwasili uwanjani hapo, Mbunge wa zamani wa Arusha, Godbless Lema, alisema kuandamana kwao huku mvua kubwa ikinyesha, ni ujumbe ambao wananchi wameutuma kwa watawala kuhusu ugumu wa maisha.

"Arusha maisha ni magumu sana na umaskini umeongezeka. Matumizi ya Arusha ukitaka kula wali nyama ni lazima uwe na Sh. 20,000 hadi 22,000 kwa siku. Ukiangalia mchele kilo moja ni Sh. 3,600, nyama kilo moja ni Sh. 10,000, viungo na mafuta 2,000, mkaa Sh. 2,500 nauli kama amefuata mbali si chini ya 1,500.

"Kwa hiyo mlo mmoja hapa Arusha, unagharimu Sh. 20,000 hadi 22,000 na hapo ni mtu kama anataka kula wali nyama. Mtu mwenye maisha ya chini au machinga hawezi kula mlo huo," alisema.

**LISSU NA SUKARI**

Katika mkutano huo, Lissu alisema amepewa taarifa na mfanyabiashara mmoja mkubwa jijini Mbeya kwamba walipewa kibali cha kuagiza sukari nje ya nchi, wameongeza Sh.1,000 ili wapate faida kwenye tani 300,000 ambazo serikali imewapa kibali cha kuingiza nchini.

"Sukari tani 300,000 kutoka nje inaingizwa bila kodi. Ni duty free (haina kodi), hailipiwi ushuru. Inakuwaje inauzwa Sh. 5,000 au 6,000 kwa kilo moja? Tunaambiwa wanaagiza sukari nje kwa bei ya chini na wanaongeza Sh. 1,000. Wanapata faida Sh. bilioni 300 na kila mmoja wanagawana Sh. bilioni 75," alisema.

Aidha, Lissu alisema kuna hekta milioni nane za ardhi ambayo ni misitu zimepewa wawekezaji kutoka nje kwa ajili ya kuzalisha hewa ukaa.

**HAKUNA KULALA**

Mwenyekiti Mbowe alisema wataendelea kuandamana kwa kuwa ni kielelezo cha hisia, na wanapeleka ujumbe kwa watawala kwa niaba ya mamiliomi ya Watanzania.

"Tuko tayari kuumia tupate kesho iliyo bora kuliko jana iliyopita. Tuna vyama vingi vya siasa lakini ni vyama vingapi vinaweza kusimama na kutetea ndoto za Watanzania kuwa ukweli katika kesho?" alihoji Mbowe.

Kwa mujibu wa Mbowe, nchi inaendeshwa kwa mikopo na watawala hawaleti mipango ya kuimarisha uchumi.

"Wanaleta masuala ya mikopo ndiyo maana nchi yetu leo haina dola (sarafu ya Marekani). Asilimia 70 ya biashara zinazoagizwa nje ya nchi yetu, inaagizwa na dola.

Lakini leo nchi yetu haina dola na kama nchi haina dola, basi vitu vitaendelea kupanda, kwa kuwa hamna dola na vitu vingi vinavyoagizwa nje vinategemea dola," alisema.

Katika mkutano huo wa kuhitimisha ngwe ya pili ya maandamano na majiji, Mbowe, alisema katika majiji yote waliyofanya maandamano, wametembea kilomita 166. Majiji hayo ni Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam na Arusha.

**AZIMIO LA MTWARA**

"Kesho (leo) wote tunaondoka tunakwenda Mtwara kutengeneza azimio ni kitu gani kitafanyika baada ya maandamano hayo ya mikoa hii. Tulikuwa na vyama vingi vya siasa, lakini ni vingapi vinatembea kilomita 20 kutetea haki za wananchi? Tumebaki CHADEMA pekee, hivyo kila mtu ajitahidi kukijenga chama hiki maana chama si Mbowe, bali ni mimi na wewe," alisema.

"Hawa wenzetu ni wepesi, tunawatandika asubuhi na mapema kwenye uchaguzi lakini ni pale tutakaposhikamana na kuacha kuja kwenye mikutano hii kishabiki bali katika mapenzi mema ya kudai haki na kugeuza maisha ya Watanzania," alisisitiza.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi, Tumaini Mafie na Woinde Shizza.**

# Ilivyoagwa miili ya watu 25 waliofariki ajali ya Arusha

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

VILIO vilitanda wakati miili ya watu 11 kati ya 25 waliofariki dunia katika ajali iliyohusisha magari manne jijini Arusha mwishoni mwa wiki, ilipowasili jana kwenye Uwanja wa Shekhe Amri Abeid kwa ajili ya kuagwa.

Miongoni mwa waliofariki katika ajali hiyo iliyotokea Februari 24, mwaka huu na kuagwa jana ni ndugu ambao ni mtu na mdogo wake, Garson Kishauli (18) na mdogo wake Cathbert Kishauli (7).

Shughuli ya kuaga miili hiyo iliongozwa na Waziri wa Sheria na Katiba, Balozi Dk. Pindi Chana. Baada ya miili hiyo kuwasili kiwanjani huko saa 4:05 asubuhi, baadhi ya waombolezaji walianguka na kupoteza fahamu na kusaidiwa na watoa huduma ya kwanza.

Mbali na ndugu Garson na Cathbert Kishali, majina ya watu wengine waliofariki dunia katika ajali hiyo na miili yao kuagwa jana ni Neema Loserian (44) na mwanawe Dorcas Loserian (2), Obedi Kimanyu (40) ambaye ni dereva wa gari la Shule ya New Vision, Elias Saning'o (27), Joseph Muna (33), Neema Loserian (44), Vicent Kazungu, Queen Lomayani (28), John Mukolwe na Judith Daud (25). "Msiba huu ni wetu sote, hivyo serikali itashirikiana na waombolezaji hadi wanapohifadhi wapendwa wao," alisema Waziri Pindi wakati akiwasilisha salamu za serikali.

Alielekeza kila mwili utakapopelekwa kuzikwa, viongozi wa ngazi za mtaa, vijiji, vitongoji na kata hadi wilaya washiriki maziko hayo.

Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Misaille Mussa, alisema katika ajali hiyo, watu 25 walifariki dunia na wengine 21 kujeruhiwa.

Alisema kati ya majeruhi hao, wanaume ni 14 na wanawake ni saba, wakiwamo raia 10 wa kigeni kutoka mataifa mbalimbali.

Mussa alisema majeruhi hao walilazwa katika hospitali tano za mkoani Arusha ambazo ni Mount Meru (11), St. Joseph (3), Selian Ngaramtoni (4), Selian Mjini (2) na Olturmet (1). Kati yao tisa ni raia wa kigeni .

"Tunawashukuru madaktari na wauguzi wetu kwa kuwa kati ya majeruhi hawa, tumebakiwa na watano ambapo wanne ni raia wa kigeni na mmoja mtanzania.

"Wengine wameruhusiwa na mmoja kupewa rufani kwenda Hospitali ya KCMC mkoani Kilimanjaro na mmoja amepelekwa Kenya baada ya nchi yao kumwomba.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema mkoa umepata "msiba mgumu", lakini kutokana na mshikamano ulioko kwa viongozi na watu mbalimbali, wameaga miili ya watu 11 na iliyobaki imechukuliwa na ndugu zao.

Alisema Rais Samia Hassan Suluhu licha ya kutokuwa nchini wakati msiba huo ukitokea, aliagiza gharama za matibabu za majeruhi pamoja na za msiba zibebwe na serikali.

"Tutaendelea kuwa karibu na familia hizi hadi pale tutakapokamilisha taratibu za maziko. Poleni sana familia na viongozi wote serikalini wakiongozwa na Rais Samia ambaye anawapa pole sana," alisema.

Katika salamu zake za pole, Kaimu Balozi Mdogo wa Kenya nchini, Nacy Pendo Sifa, alisema msiba huo umegusa mataifa mbalimbali ikiwamo Kenya kwa kupoteza wapendwa wao.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, Dk. Stanley Hotay, akizungumza kwa niaba ya Umoja wa Makanisa ya Kikristo mkoani humo, alisema Arusha imekumbwa na misiba mikubwa mfululizo baada ya aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, kufariki dunia hivi karibuni.

"Hatujatulia umetokea tena msiba huu. Watoto na vijana wamefariki dunia, inaumiza sana na kila mtu anasema lake, lakini tumwachie Mungu. Kufeli kwa breki katika gari si akili ya mtu wa kawaida, ni gari na Mungu aliruhusu. Tunamwomba Mungu kunyamazisha umauti katika Mkoa wa Arusha.

"Hatujui ni kwanini, lakini Mungu anajua. Tunahuzunishwa na maafa yanayotokea. Tunasikitishwa na msiba huu na tunatoa pole kwa wenzetu wa mataifa ya kigeni, tujipe moyo kwa kuwa wazazi, ndugu, jamaa wanajua maumivu haya," alisema Dk. Hotay.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Thomas Ole Sabaya, alisema Arusha imepata misiba mitatu mikubwa mfululizo; ajali hiyo, wa Lowassa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hassan Wakasuvi, ambaye pia alikuwa mlezi wa chama hicho Mkoa wa Arusha.


## TANGAZO LA KUPOTEA



DAWSON BUBERWA ISHENGOMA

**Bi. STELA DAWSON ISHENGOMA** wa Goba Dar es salaam anatangaza kupotea kwa mumewe ndugu **DAWSON BUBERWA ISHENGOMA** aliyepotea Tarehe **20/06/2018.**

Ndugu **DAWSON BUBERWA ISHENGOMA** alikuwa akitokea kwenye majukumu yake ya kazi, na kupotea akiwa anarudi nyumbani kwake Oysterbay Dar es salaam.

Taarifa za kupotea kwake ziliripotiwa kituo cha polisi cha kati, Dar es salaam na kupatiwa namba **DSM/CID/PE84/2018**

Kwa yeyote atakaye muona tunaomba atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye, au apige simu kupitia namba zifuatazo:

**0762-128050 / 0659-350027**

**ZAWADI NONO ITATOLEWA KWA YEYOTE ATAKAYEFANIKISHA KUPATIKANA KWAKE**

## HABARI KITAIFA



Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Balasubramaniyan Venkadachalam (kushoto), akitoa maelezo kuhusu shughuli za kiwanda hicho kwa wafanyakazi wa Kituo cha Sheria na Haki za Bianadamu (LHRC), waliotembelea ofisi za TGL, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi wa Kituo hicho, Dk. Anna Henga na (wa pili kushoto) ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kondakta auawa akidai nauli mpya ya daladala

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

NAULI mpya ya Sh. 600 kutoka kituo kimoja hadi kingine, imekatisha uhai wa kondakta baada ya abiria Venance Ngonyani (28), mkazi wa Mtaa wa Mahenge, Manispaa ya Songea, kudaiwa kumchoma kisu shingoni na kumsababishia umauti.

Kutokana na mauaji hayo, Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma linamshikilia Ngonyani kwa tuhuma hizo za mauaji.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma, Marco Chilya, alimtaja aliyefariki dunia ni Hussein Anafi (21), mkazi wa mjini Songea ambaye ni kondakta wa daladala yenye namba za usajili T 332 BXR - Town Hiace.

Kamanda Chilya alisema tukio hilo lilitokea wakati gari hilo likitokea mjini Songea kwenda Mkuzo kupitia Msamala.

Alisema kuwa baada ya kondakta huyo kumdai Ngonyani nauli yake ya Sh. 600 ndipo abiria huyo alipodai kuwa na nauli ya zamani Sh. 500 mfukoni, kauli iliyoleta malumbano kati yao.

"Wakati daladala hiyo ikiwa bado inaendelea na safari, malumbano yaliendelea na walipofika eneo la Mkuzo, kondakta Anafi alimtaka Ngonyani atoe nauli ya Sh. 600, lakini Ngonyani akasisitiza ana Sh. 500.

"Wakiendelea kulumbana ndipo Ngonyani alipochomoa kisu kilichokuwa mfukoni mwake kisha akamchoma Anafi shingoni, jambo hilo liliwashtua abiria waliokuwa ndani ya daladala.

"Wananchi waliokuwa karibu na kituo cha daladala walifika katika eneo la tukio na kumkamata Ngonyani kisha walifanya utaratibu wa kumkimbiza Anafi katika Hospitali ya Mkoa kwa matibabu, lakini kwa bahati mbaya alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu," alisimulia Kamanda Chilya.

Kutokana na tukio hilo, kamanda huyo aliwataka wananchi kuacha mara moja tabia za kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na Jeshi la Polisi halitawafumbia macho watu wenye tabia kama hizo.

Kamanda Chilya alisisitiza kuwa atakayebainika kufanya vitendo vya kuvunja sheria, Jeshi la Polisi litahakikisha sheria inachukua mkondo wake.

# Mfanyabiashara mbaroni madai ya kuuza sukari kwa bei ya juu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MFANYABIASHARA wa duka la jumla wilayani hapa, Mayengela Mboji, amekamatwa kwa madai ya kuuza sukari kinyume cha bei elekezi iliyotolewa na serikali.

Mboji amenaswa katika operesheni iliyoendeshwa na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, baada ya kubainika akiuza bidhaa hiyo kwa Sh. 189,000 kwa mfuko wa kilo 50 wakati bei elekezi ni kati ya Sh. 140,000 na 145,000 kwa ujazo huo.

Mfanyabiashara huyo alikamatwa jana wakati msafara wa Serukamba katikati ya mji wa Manyoni na ndipo lilionekana gari lililosheheni sukari na wenye gari walipoulizwa walisema wamenunua kwa Mboji.

Baada ya kuelezwa hivyo, Mkuu wa Mkoa akiwa ameambatana na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota, walikwenda katika duka la mfanyabiashara huyo na baada ya kukagua risiti za mauzo, ilibainika kuwa alikuwa akiwauzia wateja kwa Sh. Sh.189,000 na wengine Sh.184,000 kwa mfuko wa kilo 50.

Serukamba, baada ya kumhoji mfanyabiashara huyo, aliomba asamehewe kwa madai kijana aliyemwacha dukani ndiye ameuza sukari kwa bei kubwa bila maelekezo yake. Utetezi huo ulipingwa na mkuu wa mkoa na kumwagiza mkuu wa polisi wa wilaya, aliyekuwa katika msafara huo, kumkamata.

"OCD mkamate huyu mfanyabiashara na nataka huyu awe mfano kwa mkoa huu afunguliwe kesi ya uhujumu uchumi kwa kuuza sukari bei kubwa kinyume cha bei elekezi iliyotolewa na serikali," alisema.

Serukamba pia alimwagiza ofisa biashara wa wilaya ya Manyoni kwenda katika duka la mfanyabiashara huyo kusimamia sukari iliyopo iuzwe kwa Sh.70,000 hadi 72,000 kwa mfuko wenye ujazo wa kilo 25.

Baadhi ya wananchi wa mjini Manyoni waliokuwapo eneo la tukio walisema hali ya upatikanaji wa sukari imekuwa mbaya kutokana na kutopatikana katika maduka yote na hata ikipatikana inauzwa kati ya Sh. 4,500 hadi 5,000 kwa kilo moja.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED

TAARIFA KWA UMMA

SHINDANO LA WASICHANA KATIKA TEHAMA

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inawaalika wanafunzi wasichana wote wa vyuo vikuu nchini kushiriki katika shindano la Ubunifu linalohusisha uwasilishaji wa wazo lenye ubunifu zaidi linaloleta suluhisho katika jamii, wazo linalowasilishwa linapaswa kuzingatia dhima ya Siku ya Wasichana na TEHAMA 2024 isemayo "Uongozi"

Shindano hili linalenga kumpatia kila mmoja fursa ya kushiriki, kuonesha ujuzi, na kufurahia ubunifu, uvumbuzi na hatimaye kukuza weledi wa uongozi katika TEHAMA.

**Sifa za Mshiriki**

- Awe mwanafunzi wa kike Mtanzania anaesoma katika chuo kikuu.
- Awe na ujuzi wa msingi wa kutumia programu za usimbaji (coding) Mfano: Python na R.
- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 24.
- Uanachama katika Klabu ya Kidijiti ni sifa ya ziada.

Washiriki wanatakiwa kuwasilisha maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganisho kifuatacho https://edodoso.gov.go.tz/index.php/824558?newtest=Y&lang=en

**Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 12 Machi, 2024.**

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia namba 0800008272 au barua pepe dawatilahuduma@tcra.go.tz.

Imetolewa tarehe **28 Februari, 2024**

Mha. Mwesigwa Felician
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz




Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (katikati), akishiriki kuimba wimbo wa mshikamano na Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Serikali Kuu (TUGHE) tawi la Wizara hiyo, Zepahania Motela (kushoto) na Mwakilishi wa Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Dodoma, Redempta Kisima, wakati wa mkutano wa mkuu wa pili wa Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango ataka mikakati kuongeza mapato ya kodi

**Na Jenifer Gilla**

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango ameelekeza wadau katika Jukwaa la Kodi na Uwekezaji mwaka 2024 kubuni mikakati madhubuti itakayoiwezesha serikali kuongeza mapato ya kodi ifikie angalau asilimia 15 ya Pato la Taifa.

Pia ameagiza mawaziri wa fedha wazingatie ushauri kuhusu maboresho ya sera katika uwekezaji na ukusanyaji mapato ya ndani utakaotolewa na sekta binafsi na walipakodi wote katika jukwaa hilo na kuyatumia wakati wanafanya maboresho ya sera hiyo.

Mpango aliagiza hayo jana alipofungua jukwaa hilo kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

Alisema kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita (2011/12 hadi 2022/23), makusanyo ya kodi ya nchi yamekuwa chini ya asilimia 12 ya Pato la Taifa, kiwango ambacho ni chini ya wastani wa viwango vinavyohitajika kwa nchi za bara hilo huku nchi nyingi zenye kipato cha kati na chini barani zikiwa zimevuka wastani huo.

Alisema ukusanyaji kodi unazorota kutokana na mtizamo uliojengeka kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwa mfumo wa kodi uliopo ni kikwazo katika uwekezaji na ufanyaji biashara.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za Baraza la Taifa la Biashara, wafanyabiashara na wawekezaji wamekuwa wakilalamikia mambo mbalimbali katika mifumo hiyo ikiwamo wingi wa kodi, tozo na ada, sera za kodi zisizotabirika, viwango vya juu vya kodi, rushwa na makadirio ya kodi yasiyoakisi uhalisia.

Alitaja malalamiko mengine yaliyoainishwa na TIC kuwa ni kutosomana mifumo kielektroniki hasa taasisi za utoaji vibali na leseni na huduma nyingine, pia kuwapo wa sheria na kanuni zinazokinzana na mwingiliano wa majukumu ya kitaasisi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema suala la utozaji kodi linakabiliwa na changamoto nyingi hasa kwa wafanyabiashara ikiwamo kukwepa kutoa risiti za kielektroniki kwa kutoa punguzo kwa wateja wasiochukua risiti.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara, wawekezaji na walipakodi wengine wanachukulia ulipaji kodi kama jambo la Mamlaka ya Mapato (TRA) na wakati ukweli ni kuwa ni jambo la nchi na lipo kisheria na kikatiba.

Alitaja changamoto nyingine ni kuwapo visingizio vingi kutoka kwa wafanyabiashara kama vile mfumo wa malipo upo chini au vifaa kuharibika na kutokuwa na mazingira rafiki.

Alisema serikali inafanya jitihada za kutatua changamoto hizo kwa kufungua ofisi ya migogoro ya kikodi ili kushughulikia migogoro hiyo ikiwamo ukadiriaji kodi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema serikali imejitahidi kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji kwa kuzingatia mambo ambayo wanayaangalia sana ikiwamo utulivu wa kisiasa na amani na mazingira ya kisheria na sera, hasa ulinzi wa mali sehemu mtu anapowekeza.

Alisema wawekezaji pia wanazingatia kuwapo uhakika wa soko kwa bidhaa watakazozalisha, utulivu wa kiuchumi na fedha na miundombinu ya biashara, viwango vya chini vya kodi, gharama ndogo za kuajiri wafanyakazi.

Alisema serikali imefanya maboresho na mabadiliko ya kisera, kisheria na kikanuni yanayohusu kodi katika maeneo 665 sawa na asilimia 80 ya maboresho yote katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Alisema kati ya maboresho hayo 416 yalilenga kuweka mazingira bora ya uwekezaji na biashara, hivyo nchi hiyo iko katika mazingira mazuri zaidi katika historia yake.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Juma Malik Akili, alisema kupitia jukwaa hilo wanatarajia kujifunza mambo mengi kuhusu maboresho ya sera katika uwekezaji na ukusanyaji wa mapato.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Raphael Maganga, alishauri mambo mbalimbali ya kufanywa ili kuboresha mifumo ya kodi ikiwamo TRA kuendelea kutumia weledi katika kukusanya kodi na kutoa elimu kwa walipakodi.

# PM abaini kigogo kupiga mil. 189/-, asafiri nazo kwa basi

**Na Timoth Itembe,** MARA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amebaini ubadhirifu wa kutisha katika halmashauri za mkoa wa Mara na kuagiza baadhi ya wahusika kukamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Majaliwa amebaini hayo katika ziara yake ya kikazi mkoani hapa baada ya kufika katika eneo husika na kupewa ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Akiwa wilayani Serengeti jana, alibaini kuwapo kwa ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 213.7 uliofanywa na Mkuu wa Idara ya Fedha na Uhasibu wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Saad Ishabailu.

Kutokana na madai hayo ya ubadhirifu, Waziri Mkuu alimwagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Kamishna Msaidizi (ACP) Salum Morcase, kumkamata ofisa hiyo.

Ishabailu anadaiwa kuhamisha Sh. 213,748,085 kwa awamu nne kwa njia ya uhamisho wa ndani kwa kushirikiana na watumishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na kuzitumia kwa matumizi yao binafsi.

"Mkamate huyo bwana sasa hivi aende polisi akafunguliwe mashtaka. Huyu ni wa kupeleka mahakamani moja kwa moja. DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka) aelezwe afungue jalada la mashtaka. Wale wenzake tumewapeleka mahakamani tayari sababu tulibaini walihusika na wizi kama huu kwenye Manispaa ya Kigoma mwaka jana," alisema Majaliwa jana wakati akizungumza na madiwani na watumishi wa halmashauri hiyo.

Waziri Mkuu alifikia hatua hiyo baada ya kuwaeleza watumishi na madiwani mbinu wanazotumia watumishi wachache wa baadhi ya halmashauri ambao walikuwa wanashirikiana na watumishi watatu wa kitengo cha 'Treasury Single Account' (TSA) kuiba fedha za umma.

Aliwaeleza watumishi hao na madiwani kwamba Juni 10, mwaka jana, walitumia mwanya wa kuombea kibali fedha za bakaa kwa barua iliyotiwa saini na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, Chatta Luleka, kwenda Hazina.

"Ilipofika Juni 30, walikuwa wamemaliza kutumia fedha hizo na ikabakia Sh. milioni tisa lakini kwa kuwa walishaandika barua ya kuomba kibali, bado fedha hizo zilihamishwa na kuingizwa kwenye akaunti ya halmashauri Juni 19, 2023 na aliyejua alikuwa Ishabailu peke yake na hakutoa tarifa kwa mkurugenzi, mwenyekiti wa halmashauri wala wakuu wa idara.

"Nilituma timu yangu hapa ije kufanya uchunguzi, ikawahoji baadhi ya watumishi akiwamo Ofisa Mipango wa Halmashauri, Wilfred Mwita, ambaye alisema hajui uwapo wa hizo fedha wala hawakuwa na mpango wala bajeti inayohitaji hizo fedha. Mkurugenzi wa sasa, Bwana Furaha, alipoulizwa naye alisema hajui uwapo wa hizo fedha kwani alianza kazi Agosti, mwaka jana," alisema.

Majaliwa alisema Juni 21, mwaka jana, Ishabailu alianza kufanya matumizi ya fedha hizo kwa kushirikiana na mfanyabiashara wa hapa Mugumu, Daudi Chacha, kupitia kwenye akaunti zake za NMB na CRDB kwa kupitia miamala minne ya Sh. milioni 76.3, Sh. milioni 57.7, Sh. milioni 47 na Sh. milioni 32.5.

Alisema alipoulizwa na timu ya uchunguzi, Matinde alikiri kuwa haidai fedha yoyote Halmashauri ya Serengeti isipokuwa Mweka Hazina huyo aliomba apitishie fedha zake kwenye akaunti zake kwa sababu zinahitajika haraka kwa matumizi ya ofisi.

"Aliambiwa atoe Sh. milioni 189 akamkabidhi zote Ishabailu na zilizobaki (Sh. milioni 24) akaambiwa abaki nazo. Baada ya kupokea fedha hizo, Ishabailu alipanda basi kutoka Serengeti hadi Kituo cha Mabasi cha Nyegezi, Mwanza na kumkabidhi Zablon Mponzi ambaye alisema zinatakiwa haraka na wakubwa huko Dodoma bila kuwataja wakubwa hao ni kina nani. Yeye pia alikabidhi Sh. 150 kwa huyo Zablon, ina maana alibaki na Sh. milioni 39," alisema.

**MADUDU BUNDA**

Akiwa Bunda juzi, Majaliwa alionyesha kutokuridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo ya Mara huku akisema miradi hiyo imeghubikwa na wizi wa fedha za umma na kuwaagiza mkuu wa wilaya hiyo na mkurugenzi mtendaji kudhibiti wizi huo mara moja.

Alisema vitendo vya wizi katika miradi ya umma vinarudisha nyuma utendaji kazi wa shughuli za maendeleo na kusababisha wananchi kukosa huduma stahiki kwa wakati na wakati mwingine kushindwa kabisa kutekelezewa miradi ya muhimu.

Akikagua mradi wa ujenzi wa mabweni la wasichana na wavulana, Majaliwa alibaini mbinu zilizotumiwa na viongozi kuficha ushahidi kuhusu wizi wa zaidi ya mifuko 600 ya saruji kwa kuwaondoa mafundi wote waliokuwa wakiendelea na ujenzi bila sababu.

Pia alisema amebaini wizi kila sehemu ikiwamo katika hospitali ya wilaya kama vile wa milango, vifaa tiba zikiwamo X- Ray na CT-Scan, huku akihoji hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wezi hao ambao wamekuwa wakirudia mara kwa mara.

HABARI KITAIFA

# Waumini wa kanisa wafungwa jela kuzuia watoto kupata chanjo surua

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MAHAKAMA ya Mwanzo ya Kalambo mkoani Rukwa, imewahukumu kifungo cha mwaka mmoja jela waumini saba wa kanisa la Whachtower kwa kosa la kukataa watoto kupewa chanjo ya surua na rubella.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Shadrack Masija, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa hukumu hiyo ilitolewa juzi baada ya washtakiwa hao kukiri kutenda kosa hilo kwa madai kuwa ndivyo mafundisho na imani yao inavyowaelekeza.

Alisema baada ya washtakiwa hao kupewa nafasi ya kujitetea, walikiri kutenda kosa hilo ndipo mahakimu wa mahakama hiyo, Elias Mkama na Suzy Mkinga, walipowatia hatiani na kumhukumu kila mmoja kifungo cha mwaka mmoja jela.

"Wakati chanjo hiyo ikiendelea kutolewa na idara ya afya wilayani Kalambo, watu hao wanadaiwa kuwazuia watoto wenye umri kati ya miezi tisa mpaka 59 kupata chanjo ya surua na rubella kwa madai kuwa kwa mujibu wa imani yao ni kosa kuchanja chanjo hiyo kwa kuwa hayo si maagizo ya Mwenyezi Mungu," alisema.

Aliwataja waliohumumiwa kutumikia kifungo hicho kuwa ni Abel Isaya (27), Misheck Simon (28), Isack Simon (26) na Yona Simon wote wakazi wa Kijiji cha Kalambo wilayani Kalambo.

Wengine ni Efeso Peter (28), Job Simon (36) na Joshua Meshack ambao wote pia ni wakazi wa Wilaya ya Kalambo mkoani humo.

Wakati watu hao wakihukumiwa kwenda jela, Kamanda Masija alisema waumini wengine saba akiwamo askofu wao, wanaotuhumiwa kwa makosa kama hayo katika kijiji cha Lula Kata ya Kanda wilayani Sumbawanga, kesi yao inaendelea mahakamani.

Kutokana na adhabu hiyo, Kamanda Masija aliwataka wananchi mkoani Rukwa kutii mamlaka na mipango ya serikali kwa kuwa serikali ina nia njema na wananchi wake na wakumbuke kuwa hata mamlaka zilizopo zimewekwa na Mungu.

Pia alisema adhabu iliyotolewa dhidi ya waumini hao iwe funzo kwa wananchi wote kuwa wanapokiuka sheria watachukuliwa hatua.

# Bibi apandishwa kizimbani kuunguza makalio wajukuu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Mtaa wa Kagera, Anastazia Maziku (62), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita kwa mashtaka ya kuwachoma moto wajukuu wake wawili kwenye makalio na kuwasababishia majeraha na maumivu.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Nyakato Bigirwa na aliposomewa mashtaka yake, alikana kuhusika na makosa hayo na yuko nje kwa dhamana.

Masharti ya dhamana yalihusisha kuwa na wadhamini wawili ambao walitakiwa kuwa na barua za utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tatu kila mmoja.

Upande wa Mashtaka uliongozwa na Mawakili wawili wa Serikali Kabula Benjamin na Godfrey Odupoy ambao walidai mahakamani huko kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Bigirwa alimwuliza mshtakiwa kama yuko tayari kusomewa maelezo ya awali, akidai alikuwa tayari. Hakimu Bigirwa alimwambia Wakili wa Serikali Godfrey Odupoy amsomee mshtakiwa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Odupoy alidai kuwa siku ya tukio hilo Septemba 22, 2023, mshtakiwa aliwatuma wajukuu wake wawili, mkubwa ana umri wa miaka 10 na mdogo ana umri wa miaka saba (majina yao tunayahifadhi kwa kuwa ni watoto) kwenda kuchaji simu.

Walipochelewa kurudi, alikasirika na kuchukua moto na kuwachoma makalio ya wajukuu wake wote wawili na kuwasababishia majeraha na maumivu makali.

Aliendelea kudai mahakamani huko kuwa baada ya tukio hilo, baba mzazi wa watoto hao, Shukrani Jumapili alikwenda Kituo cha Polisi Geita na kufungua shauri, akipewa Fomu Na. 3 ya Polisi (PF3) kisha kuwapeleka watoto wake wote wawili katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Geita kwa ajili ya matibabu.

Alidai kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Geita na alipohojiwa, alikiri kuhusika na makosa yote mawili na baada ya upelelezi kukamilika alifikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Wakili Odupoy alidai kuwa upande wa Jamhuri unatarajia kupeleka mahakamanio huko mashahidi 10 na vielelezo vinne na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Machi 20, mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa Jamhuri.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Odupoy alidai mahakamani huko kuwa Septemba 22, 2023, mshtakiwa aliwachoma moto wajukuu wake wawili kwenye makalio na kuwasababishia majeraha na maumivu makali. Kitendo hicho ni kinyume cha sheria za nchi.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya **Jumatatu tarehe 04-03-2024 hadi tarehe 08-03-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Taveta border/ Horiri border** kuelekea **Kilombero** kupitia **Arusha, Manyara, Dodoma**, kupitia **Morogoro,** gari hizo zina namba za usajili: **T 853 DXS /T 887 DJB, T 453 DYG /T 837 DJB**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 24.00**
   **Upana** - **mita 4.20**
   **Kimo** - **mita 5.40**
3. Njia itakayotumika: **Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro hadi Kilombero** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 02-03-2024 hadi 05-03-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga** kupitia **Mlandizi** gari hizo zina namba za usajili: **T 792 DYL / T 394 DVS, T 687 DUB / T 128 ECL**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 24.00**
   **Upana** - **mita 5.10**
   **Kimo** - **mita 5.00**
3. Njia zitakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Mzenga kupitia Mlandizi** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 02-03-2024 hadi 06-03-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga,** gari hizo zina namba za usajili: **T 112 EAG / T 879 EAU T 204 DYJ / T 881 EAU T 249 EAZ / T 499 DZX**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 24.00**
   **Upana** - **mita 7.20**
   **Kimo** - **mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port, hadi Mzenga kupitia Morogoro Road** Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri) kutoka Dar-Es-Salaam Port mpaka Mlandizi,***Kutoka **Mlandizi Kwenda Mzenga** gari itasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
28.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi tarehe 02-03-2024 hadi 06-03-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Mzenga,** gari hizo zina namba za usajili: **T 116 EDS / T 310 DDH T 262 EDD / T 390 DHQ T 327 EDD / T 777 AQR T 331 EDD / T 572 EAZ**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 24.00**
   **Upana** - **mita 7.40**
   **Kimo** - **mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port, hadi Mzenga kupitia Morogoro Road,** Gari zitasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** kutoka **Dar-Es-Salaam Port mpaka Mlandizi**
   Kutoka **Mlandizi Kwenda Mzenga** gari itasafiri muda wa mchana ***(Kuanzia saa12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tatizo umeme sasa nafuu, nguvu zihamie kwenye maji

**KWA** takribani miezi sita, Tanzania ilikumbwa na uhaba wa umeme hali iliyosababisha kuwapo kwa mgawo katika maeneo mbalimbali nchini. Hali hiyo ilisababisha baadhi ya shughuli kusuasua kutokana na kukosekana kwa nishati hiyo muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Watu walilazimika kutumia majenereta katika uzalishaji hali iliyowafanya kuingia gharama kubwa katika uendeshaji wa shughuli zao. Hali hiyo pia ilisababisha serikali kupitia Wizara ya Nishati na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutupiwa lawama na hata baadhi ya wananchi wakitoa kauli mbalimbali kwamba wahusika waachie ngazi kwa kushindwa kutimiza mahitaji ya huduma hiyo muhimu.

Kuwapo kwa mgawo huo kulikotokana na baadhi ya vyanzo vya umeme kama mabwawa ya uzalishaji kupungua kina pamoja na kufungwa kwa baadhi ya mitambo ya gesi, serikali ilifanya kila juhudi kuhakikisha tatizo hilo linapungua au kumalizika kabisa.

Pamoja na kuanza kuongezeka kwa kina cha maji katika mabwawa kutokana na mvua kubwa iliyonyesha mwishoni mwa mwaka jana na mwanzoni mwa mwaka huu, serikali ilielekeza nguvu zaidi katika kuhakikisha Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere (JNHPP) linajazwa na kuruhusu baadhi ya mitambo kuunganishwa katika gridi ya taifa.

Hatimaye Februari 25, mwaka huu, kitendawili kiliteguliwa baada ya megawati 235 kuingizwa kwenye gridi ya taifa kwa kuwashwa mtambo namba tisa katika bwawa hilo. Bwawa hilo litapokamilika kujazwa maji na mitambo yote kuanza kufanya kazi, litakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.

Kutokana na kiasi hicho kuingizwa katika gridi ya taifa, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema upungufu umeme uliokuwapo wa megawatt 200 hadi 400 umemalizika na sasa kuna ziada ya megawati 70.

Waziri Biteko pia alibainisha kwamba mwezi ujao, megawati zingine 235 zitaingizwa kwenye gridi hivyo kumaliza kabisa tatizo hilo nchini. Aliongeza kuwa jitihada pia zinaendelea katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vingine ili kulifanya suala la kutokuwapo kwa umeme linabaki historia.

Kwa suala la umeme, serikali inastahili pongezi kwa kuwa ni matumaini kwamba uzalishaji katika viwanda na shughuli za kijamii zinazohitaji umeme sasa hazitakuwa na changamoto tena.


Pamoja na hayo, kuna tatizo la maji katika maeneo mbalimbali kutokana na sababu mbalimbali, hali ambayo inaipasa Wizara ya Maji na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kulivalia njuga na kulitafutia suluhu ya kudumu.

Katika mkoa wa Dar es Salaam, kwa mfano, kuna maeneo yamelalamikia kukosa maji kati ya wiki mbili hadi mwezi na hata yakitoka yanapatikana kwa saa chache na kutoweka.

Hali hiyo inaathiri baadhi ya shughuli kukwama na hata kuwapo hatari ya kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu na magonjwa ya kuhara na kuhara damu. Sababu kubwa ni kwamba kukosekana kwa huduma hiyo muhimu, kunawafanya watu katika baadhi ya maeneo kununua maji yanayotembezwa ambayo hayana uhakika kama ni masafi au la.

Ni dhahiri kwamba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imekuwa na mikakati na miradi ya maji yenye thamani ya mabilioni ya shilingi lakini jitihada hizo hazijafua dafu kuhakikisha tatizo linapungua. Kwa mantiki huyo, mamlaka hiyo inapaswa kufanya ubunifu mkubwa na kuwa na miradi ya maji ambayo itawezesha kuwapo kwa maji ya uhakika kwa muda wote wa mwaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wapigakura wajitokeze kupokea elimu hii

Sabato Kasika

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetoa vibali kwa asasi za kiraia 11 zitoe elimu ya mpigakura wakati wa uchaguzi mdogo wa udiwani katika kata 23 za Tanzania Bara utakaofanyika mwezi ujao.

Uamuzi huo umetolewa katika kikao cha NEC cha wiki iliyopita Februari 24 jijini Dodoma, huku Mkurugenzi wake Ramadhan Kailima, akizitaja baadhi ya asasi hizo kuwa ni Tanzania Centre for Disability Development Initiatives (TCDDI) inayohusika na masuala ya watu wenye ulemavu na Youth Against Aids and Poverty Association (YAAPA), ambayo pia inawahusu vijana kwenye mambo ya afya na uongozi.

Nikirejea kwenye hoja, elimu ya mpigakura ni ya muhimu kwani inalenga kuwawezesha wananchi kuwa na uelewa kuhusu sheria, kanuni, taratibu na mchakato wa uchaguzi.

Hivyo wapigakura waichangamkie nafasi hii ili iwanufaishe.

Lakini, pia kujua wajibu wao na umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi ni jambo la msingi, vilevile elimu hiyo inalenga kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba kwa kujitokeza na kushiriki kuchagua viongozi watakaowaongoza ili kujenga demokrasia ya utawala bora.

Hivyo, ni vyema wananchi wakajitokeza kutumia fursa hiyo ili kujiongezea uelewa wa kutosha kuhusu uchaguzi kuanzia kuchagua viongozi au mwananchi kuomba kuchaguliwa.

Elimu ya mpigakura ni nyenzo na kielelezo muhimu ambacho kinamwezesha kila mwananchi kuelewa kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi na nafasi yake katika kupiga kura.

Ninaamini iwapo wananchi watapata elimu hiyo, itakuwa rahisi kushiriki katika uchaguzi kwa kujiamini ili kupata viongozi wanaowataka badala kujiweka pembeni na kudhani hawahusiki katika mchakato huo.

Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya wananchi kutoshiriki katika uchaguzi, huku wakiwa na sababu mbalimbali, mojawapo ikiwa ni kudai kwamba hata wakipiga kura wanaochaguliwa ni walewale.

Kutokana na sababu hizo na nyingine nyingi, matokeo ya kutojitokeza kwao katika uchaguzi, wanachaguliwa wale ambao wao hawawataki. Lakini kama wangeshiriki ingekuwa rahisi kuwaondoa wasiowataka.

Hivyo, ni vyema wajitokeze kupata elimu ya mpigakura, ili iwajengee ufahamu na uelewa kuhusu haki na wajibu wao kushiriki katika mchakato wa uUchaguzi wakiwa na taarifa kamili na sahihi kuhusu mchakato mzima wa jinsia ya kupata viongozi wanaowataka.

Elimu ya mpigakura inahusisha pia usambazaji wa taarifa, vielelezo na vipindi mbalimbali katika vyombo vya hyabari ambavyo vinalenga kuwaelimisha wananchi kuhusu mchakato wa uchaguzi.

Mchakato huo unahusisha uandikishaji wa wapigakura, ugawaji wa majimbo, uwekaji wazi daftari la wapigakura, kampeni, utaratibu wa kiupiga kura na vituo vya kupiga kura.

Hayo yote mwananchi anatakiwa kuyajua kupitia elimu ya mpigakura, hivyo si ya kukosa, kwani inasaidia mtu kuhamasika na kuwa tayari kwa hiyari yake, kwa ufahamu wake na kwa kujiamini kwake kushiriki katika mchakato wa uchaguzi akiwa na mtazamo wa kukuza demokrasia.

Lakini pia ninadhani kwamba ili elimu ya mpigakura iweze kutolewa na kuwa na matokeo chanya, ni vyema kufanya uchambuzi na kutambua makundi ambayo yanalengwa kupatiwa elimu hiyo.

Ninatambua kuwa NEC imeyagawa makundi maalum katika sehemu kuu nne yakiwamo yaliyojitenga kutokana na sababu za kijiografia na shughuli za kiuchumi, yasiyojua kusoma na kuandika na yale yatokanayo na sababu za kimaumbile, yote hayo ni muhimu yafikiwe na elimu hiyo.

Iwapo elimu ya mpogakura itafikia makundi yote, itakuwa ni rahisi kila mwananchi kushiriki katika uchaguzi, huku akitambua kuwa ni haki yake kuchagua kiongozi anayemtaka badala ya kujiweka pembeni.

## Ziara ya kushtukiza ya waziri yabaini 'madudu' wawekezaji

**Na Fank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako amefanya ziara ya kushtukiza katika kampuni tatu na kuagiza wawekezaji nchini kutekeleza sheria na miongozo mbalimbali ya masuala ya kazi ikiwamo Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003.

Prof. Ndalichako alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya kuzuru kwa kushtukiza katika kampuni za usafirishaji za FAA Logistics, RAPHAEL Logistics na kiwanda cha kutengeneza viroba cha MJM Manufacturing Ltd, vyote vya jijini Dar es Salaam.

Akiwa kwenye viwanda hivyo, waziri huyo alibaini upungufu mkubwa katika usimikaji mifumo ya kulinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya magonjwa na ajali, wafanyakazi kutokuwa na mikataba, waajiri kutowasilisha michango katika mifuko ya hifadhi, kutolipa mishahara kwa wakati na ulimbikizaji madeni ya mishahara kwa wafanyakazi wao.

"Tumefanya ziara ya kushtukiza na tumebaini changamoto mbalimbali kwa wafanyakazi wa maeneo haya ya kazi, hivyo basi ninapenda kutoa wito kwa waajiri na wawekezaji wote kuhakikisha wanazingatia sheria na miongozo mbalimbali ya masuala ya kazi.

"Baada ya ziara hii ninaziagiza taasisi za OSHA, WCF, NSSF na Idara ya Kazi kurudi mara moja kuendelea na ukaguzi mpaka kufikia Ijumaa ya Machi Mosi ili kushughulikia changamoto hizi kwa kuainisha wafanyakazi wangapi ambao michango yao haiwasilishwi katika mifuko ya hifadhi za jamii na wangapi hawakatwi kabisa lakini pia kushughulikia usimikaji mifumo madhubuti ya masuala ya usalama na afya mahali pa kazi.

"Pia mfanye ukaguzi ili kutambua malimbikizo ya mishahara na stahiki zingine pamoja na wafanyakazi wasio na mikataba ili baada ya ripoti ya ukaguzi huu tutoe amri tekelezi kwa wawekezaji hawa na ndani ya siku 30 tuweze kufikia makubaliano juu ya utatuzi wa changamoto hizi," aliagiza.

Prof. Ndalichako aliwataka wafanyakazi katika maeneo yote ya kazi kutoa ushirikiano wa kueleza changamoto zinazowakabili bila uoga huku akielekeza waajiri kuacha mara moja tabia ya kuandama wafanyakazi wanaoeleza changamoto zao wakati wa ziara za viongozi mbalimbali.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda alisema usafirishaji ni sekta yenye mchango mkubwa katika uchumi wa nchi, lakini imekuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali, hivyo ziara hiyo ililenga kubaini changamoto hizo na kuona namna gani zinaweza kutatuliwa.

Alisema kuwa kwa upande wa masuala ya usalama na afya katika kampuni hizo, wakaguzi wa OSHA wamebaini kuna upungufu mkubwa katika utekelezaji sheria na miongozo ya masuala husika na tayari wametoa hati ya maboresho kwa wawekezaji hao.



Mkazi wa Mhunda, wilayani Magu mkoani Mwanza, akivuka mto kwenda upande wa pili kwa ajili ya shughuli za kilimo hivi karibuni, ambapo mto huo unatajwa kujaa maji wakati wa mvua na kukatisha mawasiliano ya eneo hilo kutokana na kutokuwepo kwa daraja la kuunganisha eneo hilo. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Bei ya petroli, dizeli kushuka

**Na Mary Geofrey**

BEI ya dizeli na petroli inatarajiwa kushuka kwa kipindi cha miaka miwili ijayo kutokana na serikali kuanza ujenzi wa matangi 15 ya kuhifadhi mafuta bandarini yatakayosaidia kuokoa upotevu wa mafuta na ucheleweshaji meli kushusha mizigo kutoka siku 11 hadi tatu.

Wizara ya Uchukuzi kupitia Mamlaka ya Bandari (TPA) imetiliana saini na mkandarasi M/S China Railway Major Bridge Engineering Group Co. Ltd. na M/S WUHUAN Engineering Co. Ltd ya China kujenga matangi hayo 15 ya kuhifadhi mafuta bandarini.

Mkataba huo ni kwa ajili ya mradi wa usanifu na ujenzi wa matangi na miundombinu ya upokeaji, uhifadhi na usambazaji bidhaa za mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam ambao utatekelezwa kwa miaka miwili kwa gharama ya Sh. bilioni 678.6.

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa, akizungumza wakati wa hafla hiyo iliyofanyika juzi jijini Dar es Salaam, alisema wanatarajia kuwapo uhakika wa mafuta nchini kutokana na ujenzi wa matangi hayo, gati la kupokea na kupakua mafuta ambalo pia linaweza kupunguza mfumuko wa bei na kuleta nafuu kwa mwananchi wa kawaida.

"Hii inatokana na ukweli kwamba kupanda kwa bei ya mafuta kunasababisha kwa kiasi kikubwa kupanda kwa bidhaa nyingine, kwa maana hiyo matangi haya yatakuwa na unafuu kwa wananchi," alisema Mbossa.

Alisema mradi huo utaondoa tatizo la upotevu wa mafuta katika bandari hiyo na kupunguza malalamiko miongoni mwa wafanyabiashara wa mafuta na kuimarisha ukusanyaji mapato.

"Kwa kuwa mafuta yote yatapokelewa na kupimwa vizuri yakiwa sehemu moja na kuwa chini ya TPA kabla ya kuyasambaza, hali hii itaimarisha udhibiti wa mapato ya serikali kwa kuzuia mianya ya ukwepaji kodi na kurahisisha ukusanyaji mapato yatokanayo na bidhaa za mafuta zinazoingia nchini," alisema Mbossa.

Alisema kuwapo kwa mradi huo pia kutaimarisha hifadhi ya mafuta na kuondoa changamoto ya sasa ambapo uwezo wa kuhifadhi mafuta nchini ni wa siku 15 kwa kutumia matangi ya kampuni binafsi.

Alisema mradi huo pia utachochea mashirika yanayoshughulika na mafuta kuanzisha kituo cha usambazaji mafuta kwenda nchi jirani kama Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na hivyo kuifanya Tanzania kuwa kituo cha soko la biashara ya mafuta.

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aliagiza usimamizi na utekelezaji wa mradi huo uzingatie muda wa mkataba na kukamilika kwa wakati ili kuondokana na usumbufu usio wa lazima.

Kuhusu mradi huo, alisema yatajengwa matangi yenye mita za ujazo wa 420,000 pamoja na miundombinu yake na kwamba matangi sita yenye uwezo wa mita za ujazo wa 30,000 ni kwa ajili ya dizeli na matangi matano yenye uwezo wa mita za ujazo 30,000 ni kwa ajili ya petroli.


Alisema matangi matatu yenye uwezo wa mita za ujazo 30,000 ni kwa ajili ya mafuta ya ndege na tangi moja kwa ajili ya huduma za bandarini huko.

Alisema serikali ina mpango wa kujenga gati la kupokea meli za mafuta eneo la Kigamboni kwa ajili ya kurahisisha upokeaji na usambazaji huduma hiyo nchini.

Mwenyeki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alipongeza juhudi hizo za serikali kutekeleza mradi huo na kuhimiza matumizi sahihi ya fedha za mradi na kumtaka mkandarasi kuzingatia muda wa kukamilisha mradi huo ili kuepuka hasara.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Zitto atoa ujumbe mzito kwa upinzani

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Chama cha ACT - Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema siasa za upinzani nchini kwa kiwango kikubwa zimejielekeza katika mapambano madogo yanayoathiri malengo makubwa ya kuwa na vyama hivyo.

Amesema ikiwa wanasiasa wa upinzani wataacha mapambano madogo na kusimamia masuala ya msingi ya kuanzishwa kwa vyama hivyo, kutatoa nafasi kubwa ya kukiondosha madarakani chama kinachoshika dola kwa sasa. Zitto alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana wakati wa hafla ya kumuaga iliyoandaliwa na wajumbe wa Baraza Kivuli la Mawaziri la chama hicho kufuatia kiongozi huyo kumaliza muda wake wa uongozi kwa mujibu wa Katiba ya ACT Wazalendo.

Alisema imekuwa kawaida wafuasi na viongozi wa vyama vya upinzani kushambuliana kwa masuala madogo yasiyokuwa na faida kwa jamii kwa sababu zisizoweza kukidhi malengo makubwa ya kuondosha Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani.

"Nasaha yangu kwenu wakati huu mnaoniaga kwa nafasi ya kiongozi wa chama msihangaishwe na vita ndogondogo, mnaweza kujikuta mnapoteza mwelekeo wa picha kubwa tunayokusudia kuifikia.

"Huku kwenye picha ndogondogo tutaanza kubaguana, kutengana na hata kufanyiana fitina za muda mfupi, lakini hivyo vyote ni kansa, tuzuie kwa ajili ya picha kubwa ya mbele," alisisitiza.

Zitto ambaye amewahi kuwa mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (CAG), alionya wanachama wa ACT Wazalendo kujiepusha na mazingira ya kukataa migongano ya kimawazo pale wanapotaka kufikia uamuzi mbalimbali. Chama hicho ni zao la migongano ya mawazo yaliyokataliwa maeneo mengine.

"Kwetu mtu unaweza kuwa na wazo zuri, lakini kama likikataliwa kwa hoja huwezi kulazimisha. Mfano, hili Baraza la Mawaziri Kivuli lilikuwa wazo la mwaka 2019 na ikakataliwa katika ngazi ya Kamati Kuu kwamba halina sababu yoyote.

"Lakini hatukuchoka na baada ya uchaguzi wa 2020 ilionekana ni lazima tuwe na kitu tofauti kitakachowezesha kuendesha siasa tofauti, nayo ilichukua mwaka mzima hatimaye ikakubaliwa 2022.

"Kiongozi wa chama hiki kazi yake kubwa ni kuzielezea sera za chama na kama hujajibidiisha inakupoteza katika ramani ya kisiasa hasa ukiwa na baraza kivuli kwa kuwa inatoa nafasi ya yale uliyopaswa kuzungumzia na kuonekana yakienda kufanywa na wengine kwenye baraza," alisema.

Akizungumzia wakati mgumu katika chama hicho, Zitto alisema moja ya mambo yaliyompa wakati mgumu katika uongozi wake ndani ya chama hicho ni kuondoka kwa baadhi ya viongozi wa chama, hali iliyomfanya awe anajifungia msalani na kulia.

Alisema kipindi hicho kigumu kwa chama kilikuwa kati ya mwaka 2016 na 2018, baadhi ya viongozi na watu wake wa karibu walipojiengua ndani ya chama hicho na kujiunga na vyama vingine. Alikaribia kukata tamaa.

"Kipindi hiki kilikuwa kigumu sana kwangu, nilikuwa nikirudi nyumbani ninaingia msalani, ninajifungia ili Anna (mke wake), asinione, humo ninalia sana mpaka machungu yanaponiisha ninatoka," alisema Zitto Kabwe.

Akizungumzia namna alivyoondolewa CHADEMA, Zitto alisema kikubwa ni watu kushindwa kuvumilia migongano ya kimawazo huku akitolea mfano wa chama cha ANC na Chris Hani, aliyekuwa Kamanda wa Umkotho wa Sizwe aliyeamini katika fikra tofauti kwenye kuyafikia malengo ya Afrika Kusini huru.

Alisema ni muhimu watu kuvumiliana na kuelekezana pale wanapokuwa na malengo makubwa kwa kuwa ACT ya leo ni zao la kushindwa kuvumiliana na ukosefu wa busara kwa baadhi ya viongozi wa kisiasa.

"Wakati ninafukuzwa chama nilichokuwapo, yalisemwa mambo mengi sana, lakini ukikaa na viongozi wa CHADEMA na kuwauliza na nimekuwa nikiwauliza tukiwa wawili tu, 'hivi nimefanya nini kiasi cha kustahiki adhabu yangu hii kuwa ni kufukuzwa tu na si labda kuwekwa pembeni au kuonywa?" Huwa sipewi majibu," alidai.

Zitto aliongeza kuwa dhamira yake haikuwa nafasi ya uongozi pekee, bali mabadiliko ya kimfumo. Aliamua kutojiunga na chama kingine zaidi ya kuanzisha ACT Wazalendo kwa ajili ya kusimamia yale yaliyokuwa hayaaminiwi maeneo mengine.

"Dhamira yangu ya kutaka uongozi ilikuwa ni msukumo wa kutaka kufanya mambo makubwa, basi sikukubali kuzikwa na watu wengine na safari haikuwa rahisi, ilikuwa safari yenye miiba balaa, lakini sikukata tamaa na leo mnaponiaga hapa ninajivunia kusimamia ndoto ile, sikutaka nizikwe na watu wengine," alisema Zitto.

Kwenye nafasi ya Kiongozi wa Chama waliojitokeza kuwania kiti kinachoachwa na Zitto ni wanachama wawili; Dorothy Semu ambaye ni Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara na Mbarala Maharagande ambaye ni Katibu wa Haki za Binadamu na Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria.

Nafasi ya Mwenyekiti wa Chama, Babu Juma Duni ameomba kutetea nafasi yake dhidi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman anayewania nafasi hiyo. Kwa sasa Othman ni Makamu Mwenyekiti Taifa (Zanzibar).

Nafasi ya Makamu mwenyekiti wamejitokeza wagombea watatu ambao ni Isihaka Mchinjita kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar ni Ismail Jussa na Hijja Hassan Hijja.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasha mshumaa kwenye kaburi la Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, Mwitongo, Butiama mkoani Mara jana. **PICHA: OWM**

## Kampuni ya ndege yajitosa kuongeza watalii Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MWISHONI mwa mwaka jana, Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar ilitangaza kuwa idadi ya watalii waliotembelea kisiwa hicho imeongezeka kwa asilimia 110.28 kutoka 260,644 wa mwaka 2020 hadi 548,503 mwaka 2022.

Katika kuunga mkono jitihada za serikali kuongeza idadi ya watalii Zanzibar, Kampuni ya Ndege ya Jambojet imejitosa kuwekeza kwenye sekta ya anga kati ya Kenya na Zanzibar ikitarajia kuanzisha safari za moja kwa moja kati ya Zanzibar na Mombasa kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Safari za ndege za moja kwa moja hadi Mombasa zinalenga kuongeza utalii na biashara kati ya Zanzibar na Mombasa.

Uwekezaji huo pia unatarajiwa kuimarisha utalii na usafiri na kuongeza uwekezaji utakaodumisha utajiri wa kitamaduni, kidini, urithi wa kihistoria na rasilimali za uchumi wa bluu kati ya visiwa hivyo viwili.

"Zanzibar inakuwa kisiwa cha kwanza barani Afrika ambako kampuni hiyo ya ndege inafanya safari za moja kwa moja kutoka Kenya," alisema Karanja Ndegwa, Mkurugenzi Mkuu wa JamboJet.

Alisema safari za ndege za moja kwa moja kati ya Zanzibar na Mombasa zitapunguza gharama za usafiri wa anga kati ya visiwa hivyo viwili.

"Urithi na utajiri wa Zanzibar umekuwa unawavutia wasafiri kutoka Kenya na kwingineko barani Afrika, wengi wao wakiwa watalii wanaopendelea visiwa safi na urithi wa Mji Mkongwe," alisema.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, alikaribisha kampuni hiyo na kusema kuwa itaongeza idadi ya wasafiri wa kimataifa kuja Zanzibar, wengi wao wakiwa watalii na wafanyabiashara.

# Waliopisha ushoroba mbioni kulipwa fidia

**Na Mwandishi Wetu,** BUNDA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali iko katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za malipo ya wananchi waliohamishwa katika eneo la Nyatwali, wilayani Bunda, mkoani Mara, ili kupisha hifadhi na mapito ya wanyamapori.

Majaliwa aliyasema hayo juzi alipojibu swali lililoulizwa na Mbunge wa Bunda Mjini, Robert Maboto, kuhusu malipo ya fidia kwa wakazi wa Nyatwali katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Shule ya Msingi Miembeni.

"Ninaomba muwe watulivu, tathmini ilikwishafanyika na sasa serikali inakamilisha taratibu za mwisho za uhakiki ili kufanya malipo kwa wananchi wote," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu alisema kumekuwa na changamoto katika baadhi ya maeneo ambayo wananchi wamekuwa wakitakiwa kulipwa fidia. Alisema baadhi yao wamekuwa si waaminifu kwa kuwasilisha taarifa zisizo sahihi na wengine kuweka pingamizi kuhusu utaratibu wa malipo.

Majaliwa pia alizindua mradi wa maji wa Misisi -Zanzibar ulioko Kata ya Sazira ambao umegharimu Sh. milioni 733 ambao hadi kufikia Januari, mwaka huu, ulikuwa unatoa huduma kwa wakazi 152,708 wa mjini Bunda. Akitoa taarifa ya mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda (BUWSSA), Esther Gilyoma, alisema kazi ya ujenzi wa mradi huo ilihusisha tangi la maji lenye ujazo wa lita 100,000 na maji hayo yanahudumia mitaa ya Nyasura 'B', Zanzibar na Misisi, mjini Bunda.



## TASAF yajenga kivuko cha kuunganisha kata tatu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imejenga kivuko cha watembea kwa miguu kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Mtaa wa Engosengiu, Kata ya Sinoni katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Kivuko hicho ni kiunganishi cha kata tatu za Sinoni, Lemara na Engutoto.

Wakizungumza na Nipashe wakazi hao akiwamo Naomi Mollel, aliishukuru serikali kupitia TASAF kwa kuwajengea kivuko hicho akisema awali wananchi walikuwa wanashindwa kuvuka kutokana na kuwapo kwa Mto Naura kujaa maji hasa kipindi cha masika.

"Naishukuru serikali kwa kutupatia hiki kivuko, lakini pia nina ombi ikiwezekana wafanye namna kivuko kiweze kupitisha pikipiki na bajaji kwa kuwa huduma za afya tunapata Engutoto hasa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Arusha, hivyo tunavuka hapa kwenda huko," alisema.

Alisema kwa sasa wanavuka eneo hilo bila ya kukanyaga maji ila awali mvua iliponyesha walikosa sehemu ya kupita na wakati mwingine kinamama walijifungulia eneo hilo.

Mkazi mwingine Monica Christian, alisema awali kutokana na wingi wa maji mtoni walishindwa kuvuka eneo hilo pia wanafunzi walishindwa kwenda shuleni.

Mwenyekiti wa Kamati ya usimamizi wa kivuko hicho, Zablon Kitomari, aliishukuru serikali kwa kutambua umuhimu wa wananchi wa mtaa huo na kuwajenga kivuko hicho.

Alisema asilimia 90 ya wananchi wa mtaa huo wanategemea kupata huduma mbalimba za kijamii kutoka kata za Lemara na Engutoto ambapo kivuko hicho kimekuwa mkombozi kwao.

Mratibu wa TASAF Jiji la Arusha, Maria Sangana, alisema ujenzi wa kivuko hicho kilianza kujengwa mwaka 2022 na ujenzi umekamilika huku mradi ukigharimu Sh.milioni 102.5.

# Viongozi wa dini, wajasiriamali wapewa mitungi, majiko

**Na Gwamaka Alipipi**

VIONGOZI wa dini na wajasiriamali mkoani Kilimanjaro wamepatiwa msaada wa mitungi ya gesi 1,000 pamoja na majiko, lengo likiwa ni kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Msaada huo ulitolewa kwa kampuni ya Oryx Gas kwa kushirikiana na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro, Shally Raymond, ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Watanzania.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga aliwaomba viongozi wa dini kutumia nafasi zao kujikita pia katika kusaidia jamii kutambua umuhimu wa kutunza mazingira kwa kuachana kutumia kuni na mkaa.

"Unaweza kutafakari na kujiuliza kwanini mbunge na kampuni ya Oryx wameamua kuwaita viongozi wa dini kuhamasisha utunzaji mazingira? Ni kwasababu viongozi wa dini ni watu wa thamani sana," alisema Judithi.

Alisema kumwambia mtu asikate miti ni kazi ngumu lakini kupitia kiongozi wa dini ambao wanaaminika katika jamii inakuwa kazi nyepesi kumshawishi mtu asikate miti kupitia mahubiri.

Judithi alisema uharibifu wa mazingira unatokana na ukataji miti kumesababisha hata mikoa iliyokuwa na mvua nyingi kama vile Nyanda za Juu Kusini ambayo zilitakiwa kuwa na mvua kuanzia Novemba zinaanza mwishoni mwa Desemba.

Alisema ni vema kuendelea kulinda mazingira kwa ajili ya wengine na kuwahusisha viongozi wa dini.

Aidha alisema pamoja na uwepo wa changamoto zinazotokana na uharibifu wa mazingira bado kuna fursa kwa jamii kujirekebisha kwa kulinda mazingira.

Meneja mauzo wa kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Shaban Fundi aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Benoite Araman alisema kwa muda mrefu sasa wamekuwa wanajivunia kuyawezesha makundi mbalimbali kupata nishati safi ya kupikia.

"Kufanya hivyo tunaamini tunaikomboa jamii na taifa kwa ujumla wake kwani kupika kwa gesi ya Oryx kuna maanisha kuboresha afya za kinamama kwa kuepuka kuvuta moshi mbaya wa kuni na mkaa," alisema Fundi.

Kwa upande wake Sister Piala Olomi, kutoka Shirika la Masisita wa Bibi Yetu Mkoa wa Kilimanjaro alipongeza jitihada zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau kuendelea kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema wao kama viongozi wa dini wamekuwa wakishiriki kuihamasisha jamii kutoharibu mazingira na wataendelea na wajibu huo kwani madhara ya kuharibu mazingira jamii inashuhudia uhaba wa mvua na ukame



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga (wa tatu kushoto), akiwa na Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (kushoto), Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro, Shally Raymond (wa pili kushoto), Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi (wa tatu kulia) na Meneja Masoko wa Oryx, Shaban Fundi (wa pili kulia) wakimkabidhi mtungi wa gesi ya kupikia ya oryx, Sista Piala Olomi kutoka Shirika la Masista wa Bibi Yetu mkoa huo, wakati wa hafla ya kukabidhi mitungi ya kupikia ya Oryx 1000 kwa viongozi wa dini mbalimbali pamoja na wajasiriamali mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muheza wavuka lengo utoaji chanjo surua, rubella

**Na Steven William,** MUHEZA

WILAYA ya Muheza imevuka lengo la utoaji chanjo ya surua na rubella kwa watoto wilayani hapa kwa kuwafikia watoto 33,808 kati ya watoto 27,431 iliyowakusudia.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mratibu wa Chanjo na Masuala ya Takwimu wa zoezi la utoaji chanjo hizo wilayani Muheza, Shaban Seif, alisema shughuli hiyo ilikwenda vizuri kutokana na elimu ambayo wamepatiwa wazazi kushirikiana na watoa huduma.

Hivyo aliwataka wazazi kuachana na imani potofu juu ya chanjo hiyo kwa kuwa imetolewa na Wizara ya Afya na aliwahakikishia kuwa ni salama na haina madhara yoyote kwa mtoto kwa kuwa humkinga dhidi ya magonjwa hayo.

Pia alitoa rai kwa jamii kuwa bado shughuli ya utoaji wa chanjo inataendelea kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyopo wilayani humo.

"Niwaombe wazazi kuendelea kuwapeleka watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwenye vituo vya afya kwa ajili ya kupatiwa chanjo ambayo ina umuhimu kwa afya ya mtoto," alisema Seif.

Mratibu wa Chanjo Wilaya ya Muheza, Grace Mwaimu, alisema wilaya hiyo imepokea dozi ya chanjo ya surua 27,431 na kauli mbiu ya mwaka huu 'Onyesha upendo mpeleke mtoto akachanjwe.

# Jaji Mkuu: Majaji msikatishwe tamaa na wanaolalamika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amewataka majaji nchini kutokatishwa tamaa na baadhi ya watu wanaotoka mahakamani na kuanza kulalamika wakidai kuwa hawajatendewa haki.

Amesema sheria ni mizani hivyo aliyeshindwa pia anaweza akapata haki yake kwa kukata rufaa.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha siku tatu cha majaji wafawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

"Siku hizi tumezoea kuona baadhi ya watu wanatoka mahakamani wanatafuta kamera na video (waandishi wa habari) na kuanza kusema haki imepotea bila kuangalia mizani iliyokuwa mahakamani, ninawaomba (majaji) msikatishwe tamaa na wale wanaotoka mahakamani na kusema mahakamani hakuna haki wakati wameacha mizani mahakamani," alisema.

Prof. Juma aliwaomba wadau wa Mahakama waendelee kuwaelimisha wananchi kuwa haki siyo ushindi, bali haki ni ushahidi uliotolewa mahakamani, sheria iliyotumika kwenye kutoa uamuzi na mizani ambayo imetoa haki hiyo.


Aidha alisema haki ni eneo pana japo kwa siku za karibuni wanaona baadhi ya wananchi wanapotoka mahakamani wameshindwa kesi huangalia haki kwa upande mmoja tu.

Pia alisema ushirikiano na wadau ni lazima na viongozi wawasikilize wananchi na kutumia changamoto zao kufanya maboresho na mabadiliko.

Jaji Kiongozi Mustapher Siyani, alisema idadi ya kesi za mlundikano katika mahakama hizo umepungua kutoka mashauri 878 mpaka 455 katika mahakama za hakimu mkazi na kutoka mahakama za wilaya na za mwanzo kutoka 19 hadi sifuri.

Alisema tangu kufanyika kikao kazi kama hicho mwaka 2022 muda wa wastani unaotumika tangu shauri kufunguliwa mpaka kumalizika umepungua kutoka siku 321 hadi 262.

Kadhalika alisema mlundikano wa idadi ya mashauri umepungua kutoka asilimia tano hadi mbili.



# Zahanati iliyokamilika miaka mitatu iliyopita yatelekezwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAHANATI ya Kijiji cha Bukoba Kata ya Isagehe Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, iliyojengwa kwa nguvu za wananchi na kukamilika mwaka 2020 haijaanza kutumika mpaka sasa.

Hali hiyo inawalazimu wananchi wa Kijiji hicho kutembea kilometa 10 kufuata huduma za afya katika mkoa jirani wa Tabora.

Ujenzi wa zahanati hiyo ulianza mwaka 2017 hadi 2019 kwa wananchi kuchangishana Sh.16,000 kwa kila kaya na kufanikiwa kupata Sh.milioni nane zilizotumika kujenga boma na mwaka wa fedha 2020/2021 ilikamilishwa na halmashauri kupitia fedha za ruzuku zinazotolewa na serikali.

Wakizungumza na Nipashe, mkazi wa kijiji hicho, Laurencia Amosi alisema tangu jengo hilo limekamilika mpaka sasa hakuna huduma inayotolewa na badala yake wanalazimika kufuata huduma mkoani Tabora au Kituo cha Afya Isagehe, huku wajawazito wakishindwa kuhudhuria kliniki kwa wakati wote.

Amosi alisema gharama za usafiri wa pikipiki nyakati za usiku kusafirisha mgonjwa ni Sh.10,000 hadi Sh. 15,000 na kwa gari ni Sh.30,000 hadi Sh.50,000.

Alisema nyakati za mchana kwa pikipiki ni Sh.5,000 na wale wasiokuwa na uwezo huo hususani ni wajazito hulazimika kujifungulia nyumbani na kuhatarisha usalama wa watoto pamoja na maisha yao.

Mkazi mwingine, Matha Yohana alisema, mwaka jana majira ya saa sita usiku ndugu yake alijifungulia njiani kando ya daraja wakati wakielekea Kituo cha Afya Isagehe na bahati mbaya alipoteza kichanga chake kwasababu ya kuchelewa kupata huduma na kurejea nyumbani.

Hivyo aliiomba serikali kuingilia kati suala hilo ili zahanati yao inanze kutoa huduma.

Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijiji na Mjini Manispaa hiyo, Mashala Mboje alisema mwaka wa fedha 2022/2023 halmashauri ilitenga Sh.milioni 69.140 kupitia fedha za huduma ya jamii kutoka mgodi wa Barrick Buzwagi.

Alisema kati ya fedha hizo Sh.milioni 57 zilitumika kununua vifaa tiba ambavyo tayari vimenunuliwa na Sh.milioni 12.140 kwa ajili ya ukamilishaji wa kichomea taka, shimo la kondo, ukamilishaji wa vyoo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba alitaja sababu ya zahanati hiyo kutokuanza kutumika licha ya kukamilika na kusalia kichomea taka, shimo la kondo, vyoo na nyumba ya mganga kuwa ni ukosefu wa wahudumu wa afya.

Alisema vifaatiba vipo tayari na kuahidi kutafuta wahudumu ili kabla ya Machi kuisha huduma ziwe zimeanza kutolewa na kuwa mwaka huu wametenga Sh.milioni 380 za ukamilishaji wa zahanati saba na wataanza na Zahanati ya Nuja na Bujika.

## PPRA yawaita vijana kuchangamkia mikopo 30%

**Na Jenesta Jasson,** BUKOBA

MAMLAKA ya Uthibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeyaita makundi maalum wakiwemo vijana, wanawake, walemavu na wazee kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia 30 inayotolewa na mamlaka hiyo.

Wito huo umetolewa juzi wakati wa semina ya kuwajengea uwezo viongozi wanawake kutoka Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera kuhusu utendaji kazi wa mamlaka hiyo kwa umma.

Ofisa PPRA, Mwanaisha Mollen alisema katika bajeti ya serikali ya ununuzi wa umma asilimia 30 zimepangwa kwa ajili ya kuwanufaisha makundi hayo kwa kuwapa mikopo na fursa mbalimbali za kazi ili kuinua uchumi wao.

Hivyo aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanawahamasisha wanachi kuunda vikundi vya shughuli mbalimbali ikiwemo biashara, ujenzi, ulinzi shirikishi ili wapate uhalali wa kujisajili katika mfumo wa PPRA ili kuwezeshwa au kupata mikopo kulingana na kazi zao.

Meneja Kiongozi wa PPRA, Winfrida Sanga alisema serikali inafanya manunuzi ya umma kupitia kodi za wanachi lakini pia inatenga asilimia 30 kwa ajili ya kuwanufaisha baadhi ya makundi ambapo asilimia 10 ni kwa ajili ya walemavu, 10 vijana, 5 wazee na 5 wanawake.

Mbuge wa Viti Maalumu mkoani Kagera, Neema Lugangira alisema wataendelea kushirikiana katika kuwaelimisha wananchi kuhusu matumizi ya mitandao ili kupata taarifa mbalimbali na kuongeza idadi ya watumiaji wa TEHAMA.

Alisema pia wataweza kuimalisha usalama mtandaoni ikiwa ni pamoja na kuyaibua makundi mbalimbali kuhakikisha wanachangamkia fursa hizo muhimu.



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Shinyanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Mabala Mlolwa wakikagua ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja katika barabara ya Mwakitolyo hadi Nyang'ombe wilayani Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Maambukizi mapya ya VVU Tabora yaongezeka

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAAMBUKIZI mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) yametajwa kuongezeka mkoani Tabora kutoka asilimia 5.1 hadi asilimia 5.6, licha ya juhudi mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo.

Taarifa ya ongezeko hilo imetolewa juzi na mwakilishi wa Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa cha Marekani (CDC) Tanzania, Dk. Mahesh Swaminathan.

Alisema ipo haja ya kuongeza nguvu katika uelimishaji sambamba na kuongeza uhamasishaji katika matumizi ya kinga ya ugonjwa huo.

Dk. Swaminathan alisema kutokana na ongezeko hilo kuna haja ya kuongeza kinga ili kwa wale ambao hawajapata wasiweze kuambukizwa pamoja na kupewa elimu ya kutosha, ili waweze kutumia kinga ya PREP ambayo itazuia maambukizi hayo.

Alisema Shirika la Menejiment na Maendeleo ya Afya (MDH) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya limeanza kuweka nguvu ya kusimamia huduma za jamii za kujipima na utolewaji wa huduma za tiba ya kufubaza VVU kwa jamii nchini.

"Tumefurahishwa na hatua iliyofikiwa na Tabora katika kutekeleza huduma binafsi ya kujipima VVU na matumizi ya PREP yamewawezesha jamii na wataalamu wa afya kupunguza maambukizi" alisema.

Alisema huduma za jamii za kupima VVU zimethibitishwa kuwa ni jambo muhimu katika kukabiliana na vikwazo vya upimaji wa jadi hasa vijijini ambako kupata huduma hiyo ilikuwa changamoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa MDH, Dk. David Sando alisema kwa wananchi ambao watakuwa hawana maambukizi wataendelea kuwapa huduma za kujikinga ili wasipate maambukizi ya VVU.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani Kitete mkoani Tabora, Honoratha Rutatisinibwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo alisema kati ya vituo vya afya 409, hospital 15 na zahanati 343 ni vituo 337 pekee ambavyo vinatoa huduma za kupima VVU.

Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, John Mboya alisema kupitia mradi huo mkoa umefanikiwa kujengewa jengo la kuhudumia watu wanaoishi na VVU, kutoa jjenereta 39, umeme jua kwenye vituo 10 pamoja na kuongeza ajira kwa watumishi wa afya 1,042, baikeli 100 pamoja na bajaji tano kwa ajili ya wahudumu.



Ukurasa 12

**MAWAKALA WA VYAMA VYA SIASA NA UMUHIMU WAO KATIKA UCHAGUZI**



Ukurasa 13

**Ilani ya wanawake ilivyo ndoano kuwanasa zaidi kisiasa**



CHADEMA YATAMBA:

# Kuona nguvu ya umma inayounga mkono maandamano ya amani

**Na Restuta James**

BAADA ya maandamano ya kupinga ugumu wa maisha, kudai katiba mpya na kupinga miswada mitatu ya sheria za uchaguzi kutikisa majiji kadhaa, CHADEMA inajinasibu kuwa Watanzania wanaiunga mkono na inajivunia mwitikio wao mkubwa kwenye kuifikishia ujumbe serikali.

Naibu Katibu Mkuu, Benson Kigaila, akizungumzia tija ya maandamano hayo anasema ni kubwa kwa vile wengi wamejitokeza na kushiriki.

"Ni dalili kwamba hawaridhishwi na maisha wanayoishi, wanataka katiba mpya na uchaguzi huru na wa haki."

Katika mahojiano na Nipashe, anaeleza kuwa maandamano hayo ya amani yanalenga kuwasilisha kilio cha Watanzania kwa serikali kushinikiza iwasikilize watu.

"Malengo ya maandamano ni mawili, mosi kuitaka serikali ije na mpango wa dharura wa kupunguza ugumu wa maisha na pili ni kumtaka Rais Samia Suluhu Hassan, asisaini miswada mitatu iliyofikishwa kwake ikitokea bungeni," anasema Kigaila.

Akizungumzia mwitikio mkubwa ambao umewaonesha viongozi wa serikali namna ambavyo wananchi hawaridhishwi na baadhi ya mambo anasema:.

"Kwa maana ya mafanikio ya maandamano; mwitikio wa wananchi unadhihirisha. Ujumbe umefika. Ni hatua gani serikali wanachukua, ni kazi yao. Sisi tumepeleka ujumbe, tutawapa muda wa kuhakikisha kwamba umeme unakuwa wa uhakika, sukari, nauli, mafuta na bidhaa zote muhimu zinashuka bei, kama hawajafanya tutapanga awamu nyingine," anaongeza Kigaila.



Benson Kigaila

Anasema CHADEMA itaenda hatua kwa hatua katika kuwaelimisha viongozi wa serikali hadi hapo watakaporidhika kwamba Watanzania wanasikilizwa na kero kutatuliwa.

Kigaila anasema nchi ina rasilimali za kutosha na serikali inakusanya kodi ambazo zikitumiwa ipasavyo, Watanzania watafurahia 'asali na maziwa.'

Kwa mujibu wa ibara ya nane ya katiba, serikali inapaswa kufanyakazi zake kwa kuzingatia misingi ya kidemokrasia, haki na kwamba lengo lake kuu litakuwa ni ustawi wa wananchi, anasema Kigaila.

"Kwa mujibu wa ibara hii, Watanzania wana haki ya kuishi maisha yenye neema na serikali inawajibika kuhakikisha hilo. Lakini haijafanya hivyo; umeme unakatika kila siku, sukari imepanda bei na maisha yameendelea kuwa magumu, pia hawatuambii sababu na mkakati nini," anaeleza.

Viongozi wa serikali kutojibu kwa ufasaha changamoto zinazowakabili wananchi, kunawaondolea sifa ya kuongoza nchi, anadai Kigaila.

"Serikali inakusanya kodi ili iwaletee Watanzania maendeleo, hizi kodi ni kwa ajili ya ustawi wa wananchi na hiki ndicho CHADEMA inasema kwenye maandamano," anaongeza.

Anasema serikali inapaswa kusikiliza wananchi na kuondoa kasumba ya 'kutegemea tume na polisi' kushinda uchaguzi.

"CHADEMA tunasema safari hii hakuna atakayekwenda madarakani kwa msaada wa tume au polisi, tunaona kwamba serikali ingekuwa inaenda madarakani kwa kura za Watanzania ingewasikiliza, lakini kwa kuwa wanajua wanategemea tume ya uchaguzi na polisi hawawasikilizi, hatutaruhusu hilo," anadai Naibu Katibu Mkuu.

Februari mosi kwenye mkutano wa waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, anasema lengo la maandamano pamoja na mambo mengine, ni kutaka mifumo imara ya kisheria na kidemokrasia nchini.

Kwa upande wake, Kaimu Katibu wa CHADEMA Kata ya Msasani, Dar es Salaam, Joseph Kalunguyeye, anasema gharama za maisha ni kubwa na zinawaumiza wenye kipato kidogo.

"Kwa mfano wachuuzi wadogo ndiyo wanaoamka kukimbizana kwenda sokoni na magengeni, hao ndiyo wanaokutana na adha ya ukosefu wa dawa kwenye hospitali, ndio wanaoshindwa kutoa michango ya shule na wanaopanga misururu kununua sukari inayouzwa ghali zaidi.

"Na changamoto zote hizi haziumizi CHADEMA peke yetu, zinawatesa hata wana CCM," anadai.

Anahoji: "Umeshaona mtu anatoka kwenye shangingi akapanga foleni kununua sukari? Umeshawaona wenye fedha wakiumizwa na ukosefu wa dawa zahanati? Wanakwenda hospitali za gharama kubwa zenye huduma bora kwa sababu wanamudu. CHADEMA tunataka huu ubaguzi uishe," anasema.

Anasema serikali ilipaswa kudhibiti bei ya petroli na dizeli kwani zinapopanda zinaathiri karibu kila kitu.

"Huyu anayeuza mafuta au anayetoa huduma ya usafirishaji haumizwi na bei ya mafuta kwa sababu anajua itamwangukia mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi maskini," anasema na kuishauri serikali ipunguze kodi ya mafuta.

Itakumbukwa kuwa Januari 24, mwaka huu, CHADEMA iliongoza maandamano ya amani Dar es Salaam yakianzia Mbezi Mwisho na Buguruni hadi ofisi za Umoja wa Mataifa (UN), Sinza karibu na Mlimani City na kuwasilisha madai yao kwa Mwakilishi Mkazi wa UN nchini, Zlatan Milisic.

Baadhi ya madai ya CHADEMA yameanza kushughulikiwa na serikali, ikiwamo kutangaza bei elekezi ya sukari ambayo inauzwa kati ya Sh. 4,000 hadi Sh. 5,000 kulingana na maeneo.

Serikali imewataka wafanyabiashara kuacha kuificha na kuiuza kwa bei ya ulanguzi; maelekezo ambayo hayajatekelezwa kikamilifu, kutokana na uhaba wa sukari unaowalazimisha wananchi katika baadhi ya maeneo kupanga msururu mrefu kuinunua kwa bei kubwa.

INAENDELEA UK. 14

# Mawakala wa vyama vya siasa na umuhimu wao katika uchaguzi



Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Jaji Jacobs Mwambegele (kulia), akiwa katika moja ya vituo vya kupigia kura. Wengine ni mawakala wa vyama. **PICHA:NEC**

**Na Mroki Mroki, NEC**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza uchaguzi mdogo wa udiwani katika kata 23 za Tanzania Bara ambao kwa mujibu wa ratiba utafanyika Machi 20, 2024.

Miongoni mwa washiriki muhimu katika uchaguzi huo ni mawakala wa vyama vya siasa, ambao ni wawakilishi wanaoteuliwa na chama baada ya kupata ridhaa ya mgombea kwa ajili ya kusimamia maslahi ya chama na anayegombea.

Kwa mujibu wa kifungu cha 58(1) na (2), cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, sura ya 292, chama kinaruhusiwa baada ya kupata ridhaa ya mgombea au wagombea kuteua na kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya majina ya mawakala wa kupiga kura siku saba kabla ya siku ya uchaguzi.

Orodha hiyo itajumuisha pia majina ya mawakala mbadala ambao watatumika iwapo wakala aliyepangwa atapata dharura.

Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 43(4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uchaguzi wa madiwani za mwaka 2020, mawakala wa kupiga kura watakiwa kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi wiki moja kabla ya siku ya uchaguzi kwa kujaza fomu namba 6, ambacho pia kitawahusu mawakala mbadala.

Kwa uchaguzi unaotarajiwa kufanyika katika kata 23 mawakala mbadala wataapa kiapo cha kutunza siri mbele ya msimamizi huyo Machi 13, mwaka huu.

Msimamizi huvitaka vyama vya siasa kuwasilisha kwa maandishi majina ya mawakala wa kupiga kura, anuani na vituo walivyopangiwa kufanya kazi.

Aidha, kanuni hizo huvielekeza vyama kuwasilisha barua za utambulisho wa kila wakala na kuainisha kituo alichopangiwa kwa msimamizi wa uchaguzi.

> Kwa uchaguzi unaotarajiwa kufanyika katika kata 23 mawakala mbadala wataapa kiapo cha kutunza siri mbele ya msimamizi huyo Machi 13, mwaka huu.

Barua ya utambulisho wa kila wakala itakayowasilishwa inatakiwa kuainisha kituo alichopangiwa na iambatishwe na picha mbili zenye ukubwa sawa na iliyopo kwenye pasi ya kusafiria zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu.

Endapo wakala hana picha anaweza kuwasilisha nakala mbili za mojawapo ya vitambulisho hivi cha mpigakura, cha taifa, leseni ya udereva na pasi ya kusafiria.

Siku ya kugawa vifaa vya uchaguzi kwa watendaji wa vituo, Msimamizi wa Uchaguzi atawapatia watendaji hao orodha ya mawakala wa kupiga kura kwa kila kituo ambayo itapaswa kubandikwa nje ya vituo kabla ya kuanza kupiga kura.

Msimamizi wa kituo cha kupigia kura haruhusiwi kuwaomba mawakala utambulisho mwingine wa ziada wanapofika katika vituo walivyopangiwa siku ya uchaguzi.

**AINA ZA MAWAKALA**

Zipo aina tatu kwa mujibu wa majukumu wanayotekeleza, ambao ni wakala wa kupiga kura atakayeshiriki katika shughuli nzima ya kupiga kura kituoni. Wengine ni wakala wa kupigakura baada ya zoezi hilo kukamilika ambaye anabadilika kuwa wakala wa kuhesabu kura.

Wakala wa kuhesabu kura anawajibika kushiriki kuhesabu kura mahala pa kuhesabu kura na wakala wa kujumlisha kura anawajibika kushiriki zoezi la kujumlisha kura.

Katika kituo cha kupigia kura wakala wa chama cha siasa atakuwa na wajibu wa kumtambua mpigakura anayetaka kupiga kura kama ndiye mwenye jina lililoandikwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura. Ikumbukwe kuwa, inashauriwa mawakala watoke katika maeneo ya karibu na vituo watakavyofanyia.

Wakala anapokuwa kituoni anatakiwa kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea au wagombea na chama. Pia kushirikiana na msimamizi wa kituo na msimamizi msaidizi wa kituo kuhahikisha mwenendo wa kupiga kura kituoni unazingatia masharti ya sheria na taratibu zilizowekwa na atatakiwa kujaza fomu namba 14 na 16 kituoni, kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi.

**MIIKO YA KAZI**

Kila mpewa jukumu au kazi hupewa na mipaka ya utekelezaji wa kazi zake na kwa mawakala wa vyama vya siasa wanayo pia wawapo katika vituo vya kupigia au kuhesabia kura.

Mawakala wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuorodhesha majina ya wapigakura kituoni. Wapo mawakala huacha kufanya kazi za msingi vituoni na badala yake huorodhesha majina ya wapigakura waliofika kituoni ni kinyume na sheria.

Mbali na hiyo, mawakala wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kutumia simu za mkononi ndani ya vituo vya kupigia, kuhesabu na kujumlisha kura.

Kata zitakazofanya uchaguzi huo mdogo na halmashauri zilipo kwenye mabano ni Kimbiji (Kigamboni), Kasingirima (Kigoma/Ujiji), Ndevelwa (Tabora), Msangani (Mji Kibaha), Fukayosi(Bagamoyo), Mlanzi (Kibiti), Utiri (Mji Mbinga) na Mbingamhalule (Songea).

Nyingine ni Isebya (Mbogwe), Kibata (Kilwa), Mshikamano (Musoma), Busegwe (Butiama), Nkokwa (Kyela), Kamwene (Mlimba), Chipuputa (Nanyumbu), Buzilasoga (Sengerema), Mhande (Kwimba), Kabwe (Nkasi), Bukundi (Meatu) Mkuzi (Muheza) na Boma, Mtimbwani na Mayomboni (Wilaya ya Mkinga).

Ikumbukwe kukosekana kwa weledi miongoni mwa mawakala kunaweza kuchochea vurugu na kufanya uchaguzi usiwe huru na wa haki.

***Mwandishi ni Ofisa Habari Msaidizi NEC***

# Ilani ya wanawake ilivyo ndoano kuwanasa zaidi kisiasa 2024/25

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wanaokusudia kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wanastahili kuwekewa mazingira ya kuanzia maandalizi bora, usawa ndani ya vyama vyao, kukomesha rushwa ya ngono na kuwa mchakato mzima wa uchaguzi unaozingatia uwakilishi wenye usawa wa kijinsia.

Ni jukumu la serikali, taasisi zake kama mahakama, ofisi ya usajili wa vyama, polisi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na mashirika watetezi wa haki na wanawake na usawa wa kijinsia kuhakikisha kwamba wanawake wako huru kufikia ndoto zao bila kukwamishwa wala kubaguliwa kwa namna yoyote, ndivyo inavyosema Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake ikimulika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu na mkuu wa 2025.

Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake, inatuma ujumbe kwanza kwa serikali, vyama vya siasa na Wizara ya Katiba na Sheria kuweka mazingira rafiki, ili wanawake wasibaguliwe, kwenye nafasi za uteuzi kupewa nafasi sawa na wanaume na sifa zizingatiwe.

Wanawake pia wanahitaji kupigwa jeki kimafunzo, kupitiwa misaada ya kifedha na kisheria na kisaikolojia, kulindwa polisi na mahakamani ili watoe ushahidi wakiombwa rushwa ya ngono na kunyanyaswa wakati wa kampeni.

Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake inayozinduliwa mwishoni mwa mwaka jana, ikitanguliwa na ilani za mwaka 2000, 2005, 2010, 2015 na 2020, ni mwendelezo wa matakwa au madai ya wanawake watetezi wa haki za kushiriki katika uongozi wa kisiasa ni ya sita inayobeba wanachotaka kukiona kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani.

Ikiandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi, ilani hiyo inasisitiza kuzingatia haki za wanawake kama zilivyoainishwa na mikataba mbalimbali ya kimataifa, kitaifa, kikanda ambayo Tanzania imeridhia, pia iliyobainishwa kwenye katiba, dira ya taifa ya maendeleo ya 2025, sera na mipango mbalimbali.

Ilani ambayo ni sauti ya wanawake inasema ni wajibu wa serikali kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili washiriki kikamilifu kwenye chaguzi bila vikwazo vinavyotokana na mifumo ya kibaguzi.

Inataka yawepo maboresho ya sheria na kanuni za uchaguzi kwa kuzingatia mapengo yaliyoainishwa na ilani.

Wanawake wanaipa jukumu Wizara ya Katiba na Sheria kuisimamia Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio, utafiti na kutathmini upungufu



Dk. Maryrose Majinge, mtiania urais 2020, kupitia CHADEMA.

unaoruhusu au kuhalalisha mianya ya ubaguzi dhidi ya wanawake.

Ilani inasema baadhi ya sheria hizo ni ile ya uchaguzi ambayo haijakazia utekelezaji wa misingi ya usawa katika kuteua wagombea unaofanywa na vyama vya siasa bila vigezo na kuzingitia usawa uliobanishwa kwenye sheria ya vyama vya siasa.

Kwenye uwakilishi kupitia viti maalumu vilivyoingiza ubaguzi dhidi ya wanawake kuingia bungeni kwa mfumo huo, wizara izingatie mabadiliko kama yalivyo ndani ya katiba pendekezwa ya mwaka 2014.

Aidha, ilani inataka wizara na taasisi zake zipitie kanuni za mwenendo wa uchaguzi, mfano kwenye maadili ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani 2015.

Kanuni maadili hazikubainisha miongozo ya kuwaweka wazi na kuwabana wasiozingatia maadili yanayohusu ukiukwaji wa haki za wanawake katika mchakato wa uchaguzi.

**MADAI KWA NEC**

Ilani ina ujumbe kwa Tume ya Uchaguzi (NEC), inaitaka kusimamia misingi ya haki, usawa, utawala bora katika kuteua wasimamizi wa uchaguzi na kuainisha mipaka na majimbo.

Aidha, kusimamia elimu ya uraia yenye kuzingatia misingi ya usawa wa jinsia na demokrasia thabiti, wakati wa kupigakura na baadaye kutoa ripoti yenye kuonyesha changamoto, mafanikio na mafunzo ikibainisha masuala ya jinsia wakati wa mchakato wote.

NEC ihakikishe watendaji wanaelimishwa kuhusu haki za wanawake katika uchaguzi kama ilivyobainishwa kwenye mikataba ya kimataifa, kikanda na katiba.

Jingine ni katika kuratibu, kuandikisha wapigakura NEC iweke mazingira wezeshi kwa wanawake kufikia vituo vya kujiandikisha kwa kuzingatia muda na umbali ili kinamama wafike vituoni na kupata maelezo sahihi ya kuandikishwa kwenye daftari la wapigakura.

Aidha, itoe elimu ya kutosha kwa kushirikiana na AZAKI kuhusu umuhimu wa kujiandikisha, na pia iangalie changamoto za wanawake kama wenye upofu, wasiosikia, wajawazito wanapata haki yao.

Vilevile, ilani inataka NEC kutoa ripoti ya magumu wanayopitia kinamama hao, ili kupata mbinu mpya za kurekebisha changamoto hizo kwenye uchaguzi mwingine utakaokuwa unafuata.

Kadhalika, tume izingatie usawa wa kijinsia kuteua watendaji wakuu kwa misingi ya kijinsia kwenye mchakato wote wa uchaguzi.

Kwenye kutoa elimu ya mpigakura, tume iingize masuala ya haki za wanawake katika elimu hiyo ikishirikiana na AZAKI, hususan zinazotetea usawa wa kijinisia.

Ilani inataka kwenye kampeni itoe ratiba rafiki kwa wagombea wanawake tena iwahakikishie kuwa na nafasi ya kunadai sera zao.

Pia isimamie hatua za kampeni, kukemea na kuchukua hatua dhidi ya wagombea wanaodhalilisha wanawake.

**TAKUKURU**

Ilani inaeleza kuwa ripoti za wasimamizi na wachunguzi wa uchaguzi uliopita, wamebaini kuwapo kwa viashiria vya ngono katika uchaguzi wote.

Hata hivyo, eneo hilo haliko wazi kwani waathirika husita kutoa taarifa hasa pale wanapotakiwa kutoa rushwa ili wapate wadhifa au kuteuliwa kwenye jukumu wakati wa uchaguzi.

"Kwa kutambua ukubwa wa tatizo hilo wanawake wanamtandao wa katiba, uchaguzi na uongozi na tapo (movement) la ukombozi wa wanawake tunadai yafuatayo kwa TAKUKURU."

TAKUKURU ishirikiane na AZAKI kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa ya ngono, kudhalilisha utu wa mwathiriki na ukiukwaji wa haki zake za msingi hasa anapolazimika kutoa ngono ili kupata haki zake.

Aidha, ishirikiane na AZAKI kuwajengea uwezo wanawake wanaowania uongozi ili wawe majasiri na kuwataja wanaoomba rushwa ya ngono ili kuvunja ukimya uliopo na kukomesha udhalimu huo.

Pia, TAKUKURU ichukue hatua dhidi ya vitendo vya rushwa ikiwamo ya ngono kwa kufikisha kesi mahakamani kwa mujibu wa sheria.

**KWA MAHAKAMA**

Ilani inasema ni wazi wanawake wagombea na wapigakura watahitaji msaada wa kisheria, ili watoe malalamiko bila vitisho.

Aidha, kesi zinazohusu rushwa ya ngono zinahitaji faragha ili waathirika wawe huru kujieleza na kujitetea, mahakama ziwalinde wanaotoa malalamiko yao, ilani inasema.

Kwa upande wa polisi, wanalitaka jeshi hilo kupokea na kupeleka mahakamani malalamiko ya wanawake, waliowania nafasi za uteuzi ndani ya vyama vyao au wagombea wa nafasi mbalimbali.

Aidha, ilani ya wanawake inaitaka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kusimamia utekelezaji wa maadili na kufuatilia ili kuchukua hatua ukiukwaji wa haki za wanawake kwenye uchaguzi.

Kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, ilani inaitaka ofisi hiyo kusimamia uzingatiaji wa sheria ya vyama vya siasa kwa kuzingatia misingi ya usawa wa kijinsia.

Ilani inaitaka ofisi ya msajili kufuatilia, ili kila chama kinachoshiriki uchaguzi kinazingatia usawa wa kijinsia, kwenye kutayarisha na kutekeleza sera za vyama, kuteua wagombea kwenye chaguzi za kitaifa na nafasi za uongozi ndani ya vyama.

Aidha, ilani inaitaka ofisi hiyo kuhakikisha kuwa raslimali za vyama wakati wa uchaguzi zinatumika kuwezesha wanawake kushiriki kikamilifu bila kubaguliwa.

PAMBAZUKO JIPYA WAZALENDO

# Wa kumrithi Zitto ni Dorothy Semu au Mbarala Maharagande




Mbarala Maharagande (kulia), alipochukua fomu ya kuwania nafasi ya kiongozi wa chama, kutoka kwa Katibu wa Kamati ya Uchaguzi, Mohamed Massaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya ACT- Wazalendo kuhitimisha mchakato wa kuchukua na kurejesha fomu za kuomba kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, kifuatacho sasa ni mchujo wa watiania na uchaguzi.

Kiongozi huyu anatarajiwa kupatikana Jumatano ijayo Machi 6, kwenye uchaguzi utakaowachagua mwenyekiti, makamu na Kiongozi wa Chama.

Mwisho wa kuchukua na kurejesha fomu ulikuwa Jumamosi Februari 24, na miongoni mwa nafasi zinazowaniwa ni ya Kiongozi wa Chama inayoshikiliwa na Zitto Kabwe anayemaliza muda wake.

Katibu wa Kamati ya Uchaguzi wa chama hicho, Mohamed Massaga, anasema wanatamani kumrithi Zitto ni wanachama wawili pekee Dorothy Semu na Mbarala Maharagande.

"Jumamosi iliyopita 24 ilikuwa mwisho wa kuchukua na kurejesha fomu, ni hao wawili walijitokeza. Hivyo, ndio watakaochuana katika uchaguzi wa kumpata Kiongozi wa Chama," anasema Masaga.

Anataja nafasi nyingine ambazo wanachama wamechukua fomu kutiania kuwa ni ujumbe wa halmashauri kuu, kamati kuu, viongozi wa ngome za vijana, wazee na wanawake.

Anaeleza kuwa, uchaguzi unaanza kesho kwa viongozi wa ngome ya vijana, utafuatiwa na ngome ya wazee Machi mosi na viongozi wa wanawake ni Machi 2.

"Machi 5 utafanyika uchaguzi wa wajumbe wa halmashauri kuu, ukifuatiwa na viongozi wakuu -mwenyekiti na makamu na kiongozi wa chama hapo Machi 6 na Alhamisi Machi 7, watachaguliwa wajumbe wa kamati kuu ya ACT- Wazalendo na kuhitimisha kupata viongozi watakaotumikia kwa miaka mitano." Katika mahojiano na watiania wa Kiongozi wa Chama kwa nyakati tofauti, Dorothy Semu, anaeleza kuwa rekodi bora ya utendaji anaamini itambeba.

Dorothy Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Bara, anasema tangu ajiunge na chama hicho 2014, amekuwa akipanda ngazi katika nafasi mbalimbali za uongozi kuonyesha ana sifa.

Anasema, inampa imani kuwa ni mtendaji bora anayeaminiwa na chama na sasa ni wakati mwafaka kushika wadhifa wa juu wa chama wa kiongozi wa chama.

Mtiania huyo anasema alipojiunga na chama hicho, alichaguliwa kuwa Katibu wa Sera na Utafiti, 2015 wakati chama kikiwa na mwaka mmoja alishiriki kutengeneza ilani ya kwanza ya chama.

Dorothy anafafanua kuwa 2015 chama hicho kilipata usajili wa kudumu na kushiriki katika uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huo.

Anaeleza kwa kujiamini kuwa, tangu mwaka huo, ameendelea kushika nafasi mbalimbali ikiwamo kukaimu nafasi ya Katibu wa Fedha na Katibu Mkuu, baadaye akathibitishwa kuwa Katibu Mkuu wa chama.

"Baadaye niliwania nafasi ya Makamu wa Mwenyekiti Bara ambayo ninayo hadi sasa. Nilishinda kwa kishindo wagombea wengine sita wanawake tukiwa watatu na wanaume wanne," anakumbusha.

Aidha, anasema, baada ya kifo cha mwenyekiti wa chama taifa, Maalim Seif Shariff Hamad, alikaimu nafasi hiyo hadi uchaguzi ulipofanyika mwaka 2022, Juma Haji Duni akachaguliwa kuongoza jahazi.

"Kwa hiyo ukifuatilia, utagundua kuwa tangu nijiunge na chama nimekuwa nikipanda ngazi kutoka chini hadi juu, na sasa ninawania nafasi ya kiongozi wa chama," anasema.

Anasema, amefanya kazi vizuri katika vipindi mbalimbali kikiwamo cha majonzi ya kuondokewa na mwenyekiti wa chama taifa, kusimamia chama na kwamba ana uwezo wa kumudu nafasi hiyo.

"Mwanamke katika uongozi hatakiwi kubebwa, bali kuwekewa mazingira kutimiza malengo aliokusudia ili kukabiliana na kila aina ya vikwazo, ashinde kwa uwezo wake na si vinginevyo," anasema.

**KUSIMAMIA YA HAMAD**

Mtiania Mbarala Maharagande, anasema, akiwa Kiongozi wa Chama, atatumia njia mbalimbali kushinikiza utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya Seif Shariff Hamad (marehemu) na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kuimarisha serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Bila kueleza zaidi, anasema yapo makubaliano baina ya SMZ na ACT-Wazalendo, yaliyofikiwa wakati Maalim Seif, alipokuwa Makamu wa Kwaza wa Rais wa SUK, ambayo anasema atayasimamia.

Mharagande anasema, baada ya Zitto kujenga, kuimarisha chama, kuleta utulivu na ukomavu sasa kina hazina ya kutosha ya viongozi wa rika mbalimbali akiwamo yeye na anataka kuonyesha kipaji chake.

"Nina uwezo wa kutumia nafasi hii kusimamia malengo na madhumuni ya chama, misingi yake, falsafa na itikadi, hivyo kwa kushirikiana na viongozi wenzangu hilo litawezekana," anasema.

**MDAHALO WATIANIA**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi Mkuu wa chama hicho, Joran Bashange, anasema kabla ya uchaguzi, chama kitafanya midahalo mbalimbali kwa watiania kujinadi.

Anaeleza kuwa mdahalo wa ngome ya vijana ulitarajiwa kufanyika jana, kisha leo kwa ngome ya wanawake na kufuatiwa na ule wa watiania katika nafasi ya kiongozi wa chama.

"Mdahalo huo utakuwa pamoja na ule wa mwenyekiti na makamu ambao utafanyika Jumanne Machi 4, makao makuu ya chama Magomeni hapa Dar es Salaam," anasema Bashange.

Hata hivyo, anaongeza kuwa licha ya chama kuwapa kipaumbele wanawake kuwania nafasi mbalimbali za uongozi bado ni wazito kujitokeza kushiriki katika vikao vya maamuzi hata vinavyowahusisha.

Anasema, chama kimepitisha sera ya jinsia na kuchukua hatua mahusus katika uchaguzi wake kikatiba na kikanuni na kwamba kina mchango mkubwa wa kusaidia wanawake kuingia katika vikao vya maamuzi.

## KUONA NGUVU YA UMMA INAYOUNGA MKONO MAANDAMANO YA AMANI

**INATOKA UK. 11**

Katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Arusha, wafuasi na wanachama wa CHADEMA wamejitokeza kwa wingi wakiwa na mabango yenye jumbe mbalimbali.

Baadhi ya mabango yalisomeka: "Tunataka katiba mpya, kikokotoo kwa polisi kiondolewe, kazi ya jeshi la polisi ni kusimamia usalama, uchaguzi 2024 usimamiwe na tume huru siyo TAMISEMI, bandari ni urithi wa Tanganyika, nauli zishuke, vyakula vimepanda bei, amani ni tunda la haki, kila kitu ni fedha kuanzia kujifungua hadi kuhifadhi maiti."

**MISWADA YA SHERIA**

Kuhusu miswada CHADEMA inayotaka Rais asiisaini kuwa sheria ni ule wa uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi na wa marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa, yote ya mwaka 2023.

Awali, rai ya CHADEMA ilikuwa ni serikali iiondoe bungeni na badala yake ipeleke muswada wa marekebisho ya katiba ili kuweka msingi ambao hautayumbishwa na sheria nyingine, hata hivyo rai hiyo haikukubaliwa.

Baadhi ya maoni ya wadau wakati wa mchakato wa kuitunga ni kuzuia wakurugenzi wa halmashauri wasiwe wasimamizi wa uchaguzi, ushindi wa urais uwe ni kwa zaidi ya asilimia 50 ya kura zilizopigwa, vyama viteue asilimia 50 ya wagombea wanawake kwenye ngazi mbalimbali na kuondoa kipengele cha kuteketeza nyaraka za uchaguzi baada ya miezi sita.

Miswada hiyo inasubiri saini ya rais ili iwe sheria na CHADEMA imemshauri asiisani, kwa maelezo kuwa haitatibu kile kilichokuwa kinalalamikiwa katika mchakato mzima wa uchaguzi.





## 'Watumishi wa umma msiwe kikwazo kwa wafanyabiashara'

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

KATIBU Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, amewataka watumishi wa umma wasiwe kikwazo cha kuwakwamisha wafanyabiashara bali watatue kero zinazowakabili ili biashara zao zikue.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya fursa za masoko na biashara kwa maofisa biashara kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Tabora yanayofanyika mkoani hapa, kuandaliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

"Sisi tuliopo katika ofisi za umma tuwe wawezeshaji wa wafanyabiashara, tusiwe wakwamishaji kwasababu sisi hatufanyi biashara, tukajifunze wafanyabiashara wanakumbana na changamoto gani, kwasababu sisi tupo maofisni hatujui changamoto wanazopata badala yake tunakaa maofisini," alisema.

DK. Mganga alisema maofisa biashara lazima watambue kuwa walengwa wasipopata kile kilichoandaliwa fursa za kibiashara zilizopo nchini hazitatumika na badala yake zitatumiwa na watu wachache wa nje na hivyo wananchi watashindwa kujikwamua na umaskini.

Dk. Mganga alisema wafanyabiashara kufanyabiashara katika mazingira yasio rafiki kunasababisha wengi kuchukua uamuzi mgumu wa kufunga biashara zao.

Alisema Wizara ya Biashara na Viwanda kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikifanya mafunzo ya uwezeshaji biashara na fursa za masoko zinazotokana na majadiliano mbalimbali baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa.

Aliongeza kuwa lengo la mafunzo hayo ni kujengeana uwezo katika taratibu za ufanyaji biashara na kujulishana fursa za kibiashara na uwekezaji ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema serikali imekuwa ikishiriki katika majadiliano mbalimbali ya kibiashara katika ngazi ya kimataifa, kikanda na baina ya nchi na nchi kwa lengo la kutafuta fursa nafuu za biashara, masoko na uwekezaji.

"Kupitia majadiliano hayo fursa nafuu za masoko zilizopatikana ni pamoja na fursa za masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) na Soko la Marekani kupitia Mpango wa African Growth and Opportunity Act (AGOA)," alisema.

Aliongeza kuwa pamoja na Tanzania kuwa na fursa na nafuu za masoko na biashara bado kumekuwa na changamoto kadhaa zikiwamo uelewa mdogo wa wadau mbalimbali nchini hususani wafanyabiashara kuhusu fursa hizo na mahitaji ya soko ikiwamo vya uasili wa biashara na ubora ambavyo ni muhimu katika kuyafikia masoko muhimu.

# Wakosa mawasiliano miezi 4, daraja Minyughe likikatika

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

WANANCHI zaidi ya 20,000 wa Kata za Minyughe na Makilawa, Wilaya ya Ikungi mkoani Singida wamekosa mawasiliano kwa miezi minne kutokana na kukatika kwa daraja la Minyughe.

Hata hivyo, serikali imeanza kurejesha mawasiliano kwa kuanza ujenzi utakaogharimu Sh.bilioni mbili.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) Mkoa wa Singida, Mhandisi Ibrahimu Kibasa, alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, kuwa daraja hilo lilikatika tangu Oktoba mwaka jana, limeanza kujengwa na utekelezaji wake umefikia asilimia 60 na linatakiwa kukamilika Mei 18, 2024.

Alisema daraja hilo litakapokamilika kitakachofuata ni kujenga Barabara ya Mtamaa-Minyughe hadi Mtavira kwa kiwango cha changarawe, kwamba katika mwaka wa fedha wa 2024/25 zimetengwa Sh.milioni 360.

"Barabara ya Mtamaa-Minyughe hadi Mtavira ambayo daraja hili lipo ni ya muhimu sana kwa wananchi wa kata za Minyughe na Makilawa kwani maji yakijaa katika daraja wanafunzi wanashindwa kwenda shule au wananchi kushindwa kufuata huduma za matibabu," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, baada ya kukagua ujenzi wa daraja hilo aliagiza juhudi ziongezwe ili likamilike kwa haraka na wananchi waanze kulitumia.

Pia aliagiza daraja hilo litakapokamilika TARURA ihakikishe barabara inachongwa ili kupitika muda wote.



Makamu Mwenyekiti wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini (ALAT), Mkoa wa Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe (kulia ), akiwa na wajumbe wa mamlaka hiyo mkoa, akizungumza alipowatembelea vijana wa kikundi cha Mshikamano Mwanakihanga wanaotengeneza gypsum, wilayani Mpwapwa jana kwa ajili ya kukagua mradi huo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# H/shauri Dodoma yaanza ujenzi ofisi ya machinga

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeanza utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanza ujenzi wa ofisi ya wafanyabiashara wadogo (machinga) ngazi ya mkoa, ili kupata sehemu sahihi ya kuendesha shughuli zao.

Oktoba 2022, Rais Samia alitangaza kutoa Sh.milioni 10 kwa kila mkoa kwa ajili ya ofisi za wafanyabiashara hao.

Akizungumza katika ziara ya Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Dodoma, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dodoma, Jumanne Sinoni, alisema agizo hilo la Rais limeanza kutekelezwa na ujenzi wa ofisi hiyo umeanza.

Alisema kuwa halmashauri hiyo ilipokea Sh.milioni 10 Aprili 2023 mwaka huu na ilielekezwa itumike kwa ajili ya kuanza ujenzi kisha halmashauri ikamilishe kwa fedha za mapato ya ndani.

Alibainisha kuwa mradi huo ulianza kutekelezwa Februari 19, mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Machi 30, mwaka huu ambapo jengo hilo litakuwa na vyumba vitatu vya ofisi, kumbi moja ya mkutano.

Aidha alisema kuwa halmashauri imetenga Sh. milioni 16 kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji.

"Kwa niaba ya machinga tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kundi hili maalum la machinga na kuwapa heshima ya kuwa na mahali pa kukutana na kushiriki katika shughuli za maendeleo," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Makole, Suzan Yohana, alisema kuwa kukamilika kwa ofisi hiyo kutawezesha wafanyabiashara kuwa na mahali pa kukutana na kujadili masuala yao.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo, Katibu wa CCM Wilaya ya Dodoma Mjini, Sophia Kibaba, alisema kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akitafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na sisi hatutamwangusha tutafuatilia bega kwa bega miradi yote inayotekelezwa tunawaomba watendaji wakae mguu sawa katika hili," alisema.

Pia alimtaka msimamizi wa mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Kata Makole kuhakikisha anaondoa mapungufu yaliyoonekana ikiwamo kurekebisha vipimo vya geti la kuingilia kwenye ofisi hizo.

Mjumbe wa kamati hiyo, Bushura Mohamed alisema kuwa miradi inayotekelezwa na serikali inatakiwa kusimamiwa vizuri kwa kuwa Rais Samia amekuwa akitoa kipaumbele Mkoa wa Dodoma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.





# Madereva bajaji waomba klabu kupambana na dawa za kulevya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAMILIKI na waendesha pikipiki za magurudumu matatu 'bajaji' jijini Mbeya wameomba Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini (DCEA) kuwasaidia kuanzisha klabu ya kupinga dawa za kulevya ndani ya chama chao.

Walitoa ombi hilo kwenye mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika juzi na kuhudhuriwa na maofisa wa DCEA ambapo walisema madereva wengi wamekuwa wakitumia dawa hizo hasa bangi hali ambayo inachafua taswira yao.

Victor Ngala ambaye ni miongoni mwa wamiliki wa bajaji alisema vijana wengi wamekuwa wakijiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kutokana na kukosa elimu ya kutosha kuhusu madhara yake.

Alisema wakiunda klabu ya kupinga matumizi ya dawa za kulevya wataitumia kutoa elimu kwa vijana hao pamoja na makundi mengine ya kijamii kuhusu madhara ya kutumia dawa za kulevya.

"Sisi kwenye chama chetu ni rahisi kuwabaini wasambazaji wa dawa hizi, watumiaji na ambao wanaanza kujiingiza, kwa hiyo tukisaidiwa kuunda klabu hizi tutakuwa tumeokoa kundi kubwa la vijana ambao wangeweza kujiingiza kwenye dawa hizi," alisema Ngala.

Alisema hata wanapotaka kukemea itakuwa rahisi zaidi wakiitumia klabu yao kuliko kila mmoja kukemea kivyake akidai kuwa wanahitaji nguvu ya pamoja.

Naye Neema Emmanuel ambaye ni miongoni mwa madereva bajaji wanawake jijini hapa alisema wapo madereva bajaji wachache ambao wamekuwa wakitumia dawa hizo lakini inakuwa vigumu kuwachukulia hatua kwa sababu ni vigumu kuthibitisha.

Alisema kitendo cha vijana hao wachache kutumia dawa hizo kimekuwa kikichafua kundi zima la madereva akieleza kuwa abiria wamekuwa wakiwajumuisha wote kuwa wanatumia dawa za kulevya.

"Mimi huwa nachukia sana ninaposikia abiria wakisema madereva bajaji mnavuta bangi, tukisaidiwa kuanzisha klabu ya wapinga dawa za kulevya itatusaidia kupunguza hili tatizo," alisema Neema.

Oscar Mwambengo aliomba chama chao kipatiwe vifaa vya kupimia watu wanaotumia dawa hizo ili iwe rahisi kuwabaini na kuwachukulia hatua za kinidhamu pamoja na kuwapatia elimu.

Alisema wakipatiwa vifaa hivyo vitawasaidia kupata uhakika wa mtu yeyote ambaye wanamhisi kuwa anatumia dawa za kulevya na kutumia njia sahihi kuwanusuru.

Mwasisi wa chama hicho jijini Mbeya, Iddy Ramadhan, alisema chama hicho kwa sasa kina zaidi ya wanachama 3,000 ambao wanafanya kazi kwa nyakati tofauti na kwamba wanahitaji elimu ya kutosha kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema kutokana na elimu ambayo wamekuwa wakiipata kutoka kwa maofisa wa DCEA wameanza kuelewa vizuri madhara ya dawa hizo na wanakusudia kuendelea kutoa elimu kwa wenzao.

Ofisa Elimu wa DCEA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Adrick Ndelwa, alisema wanaendelea kutoa elimu kwenye makundi mbalimbali ya kijamii ili kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na uelewa wa kutosha.

Alisema wameyafikia makundi mbalimbali wakiwamo wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi, sekondari na vyuo pamoja na makundi mengine yakiwamo ya waendesha bodaboda na bajaji.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dk. Francis Michael, akiwasikiliza wanafunzi wa Shule za Msingi za Katete na Mpemba, mjini Tunduma juzi, alipozitembelea kwa lengo la kukagua maendeleo ya wanafunzi na kupima uelewa wao. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

## Serikali yamaliza migogoro ya ardhi Kata ya Mbuyuni

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKAZI wa Kata ya Mbuyuni katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, wameondokana na migogoro ya ardhi baada ya serikali kuwasaidia kupima viwanja na mashamba yao na kuwasaidia kupanga matumizi bora ya ardhi.

Ofisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Remigi Lipiki ambaye anasimamia mradi wa kuwawezesha wananchi kumiliki ardhi wa wilaya hiyo aliyasema hayo wakati wa upimaji wa mashamba ya wananchi katika kata hiyo.

Alisema kwenye eneo hilo wamepima zaidi ya viwanja na mashamba 1,500 na kuwapatia hatimiliki wananchi ili waendelee kuyaendeleza maeneo yao bila migogoro ya aina yoyote.

"Hili eneo ni miongoni mwa maeneo ambayo yalikuwa yanakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi lakini kwa sasa nina uhakika hakutakuwa na mgogoro wa aina yoyote kwa sababu upimaji ulikuwa shirikishi," alisema Lipiki.

Aliwataka wananchi kuendelea kuyatumia maeneo hayo kwa mujibu wa makubaliano yao ili maeneo yote yatumike kwa mujibu wa sheria ya matumizi bora ya ardhi.

**"Hili eneo ni miongoni mwa maeneo ambayo yalikuwa yanakabiliwa na migogoro mingi ya ardhi lakini kwa sasa nina uhakika hakutakuwa na mgogoro wa aina yoyote kwa sababu upimaji ulikuwa shirikishi," alisema Lipiki.**

# Waomba serikali kupunguza uhamasishaji uzazi wa mpango

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

WAKAZI wa Kata za Ludende, Madilu na Milo zilizopo wilayani Ludewa Mkoa wa Njombe wameomba serikali kupunguza kuhamasisha matumizi ya uzazi wa mpango ili waweze kuzaliana kwa wingi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Afya, Malaria na Viashiria (Tanzania DHS-MIS 2022), ilionyesha wanawake walio kwenye ndoa na waliofikisha umri wa kuolewa (15-49) katika mikoa ya Njombe, Mbeya na Kilimanjaro ndiyo watumiaji zaidi wa njia zote za uzazi wa mpango kwa zaidi ya asilimia 50.

Aidha utafiti huo uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, ulionyesha wanawake kwenye mikoa ya Njombe wanatumia uzazi wa mapango kwa asilimia 64, Mbeya asilimia 58 na Kilimanjaro asilimia 63.

Hayo yaliibuka katika mafunzo ya matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kwa viongozi mbalimbali wa wilaya na Halmashauri ya Ludewa.

Walisema kwamba tangu serikali iwape elimu hiyo wananchi wameacha kuzaa na kusababisha vijiji vingi kuwa na mimba chache kwa mwaka na shule kukosa wanafunzi wa kutosha.

"Sisi hatuzai kwa sababu ya uzazi wa mpango ninaomba serikali ipunguze hata kidogo ili watu wazae sana itafika sehemu hatuna vijana kupitia uzazi wa mpango," alisema.

Naye Izack Mhiche alisema kuwa ni vizuri hatua za haraka zikachukuliwa ikiwamo kupunguza elimu ili kusaidia wilaya hiyo kuwa na watu wengi.

Awali akiwasilisha mada katika mkutano huo mtakwimu kutoka NBS, Hellen Chuwa alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022 Mkoa wa Njombe una watu 889,946 huku Wilaya ya Ludewa ikiwa na watu 151,361.

"Sio kwamba kwa vile mpo wachache hamtapata miradi hapana, takwimu zinarahisisha kujua ni wapi kitu kwa kiasi fulani kiende wapi," alisema Chuwa.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga alisema kuwa suala la uchache wa watu linasababishwa na vitu vingi ikiwamo kuhamahama kwenda maeneo mengine kutafuta fursa.

"Kwa hiyo sasa ili Mkoa wa Njombe idadi ya watu iongezeke dawa yake ni kuwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi kuleta miradi mingine ije huku," alisema Kamonga.

Katika hatua nyingine viongozi wa dini akiwamo, Martin Kabojoka waliishauri serikali katika sensa ijayo kuongeza dodoso la wapagani ili watumie takwimu hiyo kuwarudisha kundini.

Akitolea ufafanuzi suala hilo mtakwimu kutoka NBS, Hellen Chuwa, alisema takwimu za makabila wala za kidini hawaangalii kwa namna ya kutokuleta mkanganyiko.



# Utendaji bandari kuboreshwa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed amesema serikali imedhamiria kuboresha utendaji wa bandari visiwani hapa ili kukuza uchumi.

Mohammed alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa ushirikiano wa kufanya kazi kwa pamoja kati ya Shirika la Bandari Zanzibar na Taasisi ya Tony Blair.

Alisema serikali imeamua kuweka kipaumbele katika kukuza bahari kutokana na kukua kwa sekta ya biashara, uwekezaji, utalii na usafirishaji kama njia kuu ya kukuza uchumi visiwani hapa.

Alisema wizara yake inafuatilia Bandari ya Unguja na Pemba na jumuishi ya Mangapwani, Fumba, Malindi, Mkoani, Chakechake na Shumba kwa kuangalia gharama za uendeshaji kama zipo juu.

Waziri huyo, alisema gharama hizo ziko juu kwa sababu ya utaratibu wa uendeshaji na ukosefu wa mifumo ya usimamizi wa shughuli za bandari.

"Tulichokubaliana na taasisi hii ya Blair aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza ni kuwa na chombo kitakachosaidia kuboresha uendeshaji bandari kwa ufanisi na kueleta tija katika ukuaji wa uchumi," alisema.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuimarisha miundombinu ya bandari ili kuongeza ukuaji wa uchumi wa taifa.

Alisema hatua hiyo imesababisha kuyafanyia kazi mapungufu, upanuzi wa bandari hizo na kuweka mfumo mzuri wa uendeshaji kwa kupunguza gharama.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Akif Ali khamis, alisema wanakusudia kuondoa malalamiko ya wananchi na wafanyabiashara kwa kutoa huduma kwa viwango vya kidunia.

Mtendaji wa Taasisi hiyo, Frank Matsaert, alisema historia Zanzibar inatambulika kimataifa kuwa ni kituo kikuu cha biashara, hivyo kuziimarisha bandari hizo kutaongeza ubora wa huduma kama ilivyo kwa baadhi ya nchi za Afrika.

## Hospitali ya rufani Binguni mbioni kujengwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imepata mkopo wenye masharti nafuu wa Shilingi bilioni 418.5 kutoka Benki ya Exim ya Korea ya Kusini kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Binguni Wilaya ya Kati Unguja.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha baraza la wawakilishi na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Juma Makungu wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, Bakari Hamad Bakari aliyetaka kujua faida inayopata Zanzibar katika uhusiano wa kidiplomasia na taasisi nyingine za fedha.

Makungu, alisema ujenzi wa hospitali hiyo ni miongoni mwa miradi ya kimkakati ambayo SMZ imelenga kutekeleza katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alisema mradi huo ulikuwa utekelezwa muda mrefu, lakini ulikwama kutokana na kukabiliwa na changamoto ukosefu wa fedha.

Alisema ujenzi wa hospitali hiyo utakuwa na faida nyingi ikiwemo kutoa tiba ya kibingwa na utafiti wa magonjwa mbalimbali kwa wananchi.

Makungu alisema serikali ipo katika hatua za mwisho ya kufanya upembuzi yakinifu katika utekelezaji wa mradi huo baada ya kupata mkopo huo ambao ni sawa na dola milioni 163 za Marekani na majengo yatakayojengwa.

**Hayo yalisemwa jana katika kikao cha baraza la wawakilishi na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Juma Makungu wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, Bakari Hamad Bakari aliyetaka kujua faida inayopata Zanzibar katika uhusiano wa kidiplomasia na taasisi nyingine za fedha.**



Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu Mkutano wa Mawaziri wa Sheria wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola, unaotarajiwa kisiwani humo, Machi 04 hadi 08 mwaka huu. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman. **PICHA: MAELEZO ZNZ**

# Samia kufungua mkutano mawaziri wa sheria Madola

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kufungua mkutano wa mawaziri wa sheria wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola visiwani hapa mwezi ujao.

Samia atafungua mkutano huo Machi 4 na kufungwa Machi 8 na Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi.

Mkutano huo ambao utakuwa na washiriki 300 kutoka nchi wanachama 56 za jumuiya hiyom ikiwamo Tanzania imepata heshima kubwa ya kuwa mwenyeji ambaye ni mwenyeji wake.

Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Balozi Pindi Chana, akizungumza juzi na waandishi wa habari visiwani hapa, alisema mkutano huo ni kwanza kufanyika visiwani hapa.

Chana, alisema Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo kutokana na sifa ya amani, utulivu na kuwa na vivutio vya utalii.

Alisema Tanzania inaendelea kuwa mfano wa utawala bora kupitia muhimili wa Mahakama hasa katika utawala wa sharia na kutoa huduma za kuwapa haki wanancghi wakiwemo watoto.

Chana alitaja mkutano huo ajenda kuwa ni kuhusu haki za watu, njia ya kuzipatia ufumbuzi na kuepuka kutumia sheria mikononi.

Alisema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepiga hatua kwa kufanya maboresho ya sheria zake ili kwenda na wakati uliopo.

Waziri huyo alisema ajenda ya Tanzania katika mkutano huo ni masuala ya haki kwa wananchi na kuitaka iwe ni sehemu ya amani ili waishi kwa kufuata sheria za nchi na utaratibu na kuwa mabalozi wazuri kwa kuwatetea wasiyotendewa haki ili kupata haki zao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema mkutano huo utaipatia Zanzibar heshima kubwa kiuchumi, kisiasa na kijamii na kuleta tija kwa Taifa.

Alisema ushirikiano kwa pande mbili za Muungano katika sheria utaendelea kuimarika kwa kutoa huduma watu wenye changamoto mbalimbali, watoto na wenye ulemavu.

Kauli mbiu ya mkutano huo ni "matumizi ya kidigitali katika kutekeleza mifumo ya sheria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GETRUDE EDESS TIMIRA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0369/0788** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia RUVU GIRLS SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/14764/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HILDA JAMES MHANGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2210-0005** kilichotolewa na **ECKERNFORD CAMBRIDGE SECONDARY** mwaka 2011. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S2499-0623** kilichotolewa na TUSIIME SECONDARY mwaka 2014. Cheti cha Chuo Kikuu chenye namba **BLGM 1403265-14** cha MZUMBE UNIVERSITY - MOROGORO mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa za polisi: **PHQ/DAR/KIN/24778/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MTOA MWANDEGE MTOA** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha nne chenye index namba **S1633/0187** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **OLD TANGA SECONDARY SCHOOL MWAKA 2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/UBU/27216/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ELESIA THOMAS NDAWALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki matairi matatu (GUTA) yenye namba ya usajili **MC 673 BEV.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/TAN/MUH/1605/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAPTIST MISSION OF TANZANIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER HARD TOP** yenye usajili namba **T 490 BYW.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA :

**PHQ/DAR/KIN/27086/2024**

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 45/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: GEOFREY STEPHEN MBEO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: GEOFREY STEPHEN MBEO**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**UNATAKIWA KUFIKA KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI BILA KUKOSA SIKU HIYO MADAI YA TSH. 12,904,738/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 18 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **21st Mwezi wa 2 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 39/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: NAJMA HASSAN BASEBE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: NAJMA HASSAN BASEBE**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 28 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 5:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **27 Mwezi wa 02 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 42/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: NHIBULA FULA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: NHIBULA FULA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**UNATAKIWA KUFIKA KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI BILA KUKOSA SIKU HIYO MADAI YA TSH. 11,685,610/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 18 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo **tarehe 4 Mwezi wa 2 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BAGAMOYO**

**Kituo cha KEREGE Mkoa wa PWANI**

**Shauri la Madai Na. 7/2024**

**Jina la madai: MWITA MOBINI GEKORI**

**Jina la mdaiwa: ELIUD CHAGORA GEKORI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ELIUD CHAGORA GEKORI**

Kwa kuwa Mdai/Wadai/Ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
KUJA KUJIBU MADAI YA TSHS 103,883,015.55/=
OMBI LA ZUIO LA A/C 23510009647 NA OMBI LA KUWA MSIMAMIZI MPYA WA MOBINI G. GITANO
Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 4 Mwezi 3 Mwaka 2024 saa 3:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mshahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 23 Mwezi wa 2 Mwaka 2024.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO KEREGE BAGAMOYO

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 3196 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: GODSON DAIMON MBULI**

**By 1: AIKANDE NDESANJO MASSAWE**
**2: _______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 18 day of March.2024

Dated at.....this **20 day of Feb.2024**

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE INCHARGE DISTRICT COURT

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 46/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: ABOLEL KIBOMA PAUL**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ABOLEL KIBOMA PAUL**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**UNATAKIWA KUFIKA KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI BILA KUKOSA SIKU HIYO MADAI YA TSH. 17,809,331/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 18 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **21 Mwezi wa 2 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 39/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: NAJMA HASSAN BASEBE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: NAJMA HASSAN BASEBE**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 28 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 5:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **27 Mwezi wa 02 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 44/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: ABEL JOHN MWASONGWE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ABEL JOHN MWASONGWE**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**UNATAKIWA KUFIKA KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI BILA KUKOSA SIKU HIYO MADAI YA TSH. 11,071,508**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 18 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **21 Mwezi wa 2 Mwaka 2024.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

**FOMU MADAI - 3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Ndoa Na. 36/2024**

**Jina la mdai: DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa: LILIAN FADHIL MBAGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: LILIAN FADHIL MBAGA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 26 Mwezi wa 03 Mwaka 2024 saa 4:00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe ..... Mwezi wa .... Mwaka ......

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO KINONDONI WILAYA YA KINONDONI

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

HABARI KIMATAIFA

## Guterres: Hali usalama inazidi kuwa mbaya

**GENEVA,** Uswiz

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres amesema hali ya usalama duniani inazidi kuwa mbaya kutokana na makundi ya wapiganaji katika mataifa kama Jamhuri ya Kidemorasia ya Congo (DRC), Myanmar, Ukraine, Sudan na Ukanda wa Gaza kupuuza sheria za kimataifa.

Kiongozi huyo anayesimamia shughuli za Umoja wa Mataifa, alitoa wito kwa viongozi wa mataifa mbalimbali kujitolea kwa ajili ya amani na usalama duniani kote na kuheshimiwa kwa haki za binadamu.

Akizungumza wakati wa kikao chake cha kwanza cha baraza la haki za kibinadamu la Umoja wa Mataifa mjini Geneva, Uswiz Guterres alitahadharisha kuwa hali ya usalama inazidi kuwa mbaya duniani, hivyo kila kiongozi anawajibu wa kuhakikisha kuwa usalama unaimarika.

"Mizozo inayoendelea katika baadhi ya mataifa inawasababishia watu mateso makubwa, kutokana na kutoheshimiwa kwa haki za kibinadamu," alisema.

Guterres pia alilitetea shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA), akilitaja kama uti wa mgongo kwa juhudi za usaidizi katika ukanda wa Gaza wakati linakabiliwa na shinikizo la kutaka kuvunjwa.

"Moja ya ahadi ya ulinzi ya mashirika yote ya Umoja wa Mataifa ni kufanya kila linalowezekana kulinda watu," alisisitiza.

Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu, Volker Turk, pia alitahadharisha kuwa kazi ya chombo hicho iko hatarini kutokana na kile alichokiita kuwa majaribio ya kuendelea kudhoofisha uhalali na kazi ya UN na taasisi nyingine. **DW**

**"Mizozo inayoendelea katika baadhi ya mataifa inawasababishia watu mateso makubwa, kutokana na kutoheshimiwa kwa haki za kibinadamu," alisema.**

# Idadi ya vifo yaongezeka Gaza

**GAZA,** Palestina

WIZARA ya Afya ya Gaza imebainisha kwamba idadi ya vifo vinavyotokana na mashambulizi vimeongezeka na kufikia watu 29,878, huku wengine 70,215 wakijeruhiwa wakati huu Jeshi la Israel likisema kuwa operesheni za kijeshi bado zinaendelea katika ukanda huo.

Inaelezwa kuwa idadi hiyo imeongezeka kutokana na shambulio la jeshi la Israel katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa kimabavu, na kwamba mapigano makali pia yalitokea katika kambi ya wakimbizi ya Far'a.

Pia inabanishwa kuwa madaktari katika hospitali ya al-Shifa katika mji wa Gaza wanawahudumia waathiriwa wakiwa sakafuni baada ya wanajeshi wa Israel kuwafyatulia risasi watu waliokuwa wakisubiri msaada.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Jeshi la Israel, wanafanya msako katika eneo la Zeitoun, ambalo wanadai kuwa wamegundua vifaa vya kutengeneza silaha na kurusha roketi zinazotumiwa na Hamas.

Pia wanadai kuwa idadi isiyojulikana ya wapiganaji wa Kipalestina waliokuwa kwenye shimo la handaki katika eneo hilo na wengine katikati mwa Gaza.

Wakati hayo yakiendelea inaelezwa kuwa mazungumzo ya mkataba mpya wa usitishaji vita yanaendelea, huku Rais wa Marekani, Joe Biden akisema kuwa anatumai hadi ifikapo Jumatatu Machi 3, mwaka huu kutakuwa na usitishwaji mapigano.

**Wakati hayo yakiendelea inaelezwa kuwa mazungumzo ya mkataba mpya wa usitishaji vita yanaendelea, huku Rais wa Marekani, Joe Biden akisema kuwa anatumai hadi ifikapo Jumatatu Machi 3, mwaka huu kutakuwa na usitishwaji mapigano.**

Duru za habari zimeiambia Al Jazeera kwamba mpango huo unaweza kuhusisha wafungwa 400 wa Kipalestina na mateka 40 wanaoaminika kushikiliwa huko Gaza.

Aidha, Hamas iliukosoa utawala wa Biden kwa kuwezesha kuzingirwa kwa Gaza na kusema njaa katika eneo hilo ni aibu kwa ubinadamu na historia ya tukio hilo haitaifuta.

Katika hatua nyingine, inabainishwa kuwa Mahakama ya Haki ya Kimataifa (ICJ) juzi ilihitimisha siku sita za kesi za kusikiliza na kwamba zaidi ya nchi 50 ziliwasilisha hoja zao kuhusu matokeo ya kisheria ya uvamizi wa Israel katika Ukanda wa Gaza.

Inaelezwa kuwa mahakama hiyo sasa itazingatia hoja zilizowasilishwa na kurejea na maoni baada ya takribani miezi minne hadi mitano.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa kesi hiyo ni tofauti na kesi nyingine ya ICJ iliyowasilishwa na Afrika Kusini Desemba 29, 2023 ambayo inadai kuwa Israel inatekeleza uhalifu wa mauaji ya halaiki katika vita vyake vinavyoendelea dhidi ya Gaza. **ALJAZEERA**



Kuanzia kushoto kwenda kulia Rais wa Kenya, William Ruto, na mwenzie wa Uganda, Yoweri Museveni, pamoja na kiongozi wa upinzani Kenya, Raila Odinga, wakiwa pamoja katika shamba la Rais Museveni walipokutana kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ikiwamo diplomasia, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Museveni, Ruto wateta na Odinga

**KAMPALA,** Uganda

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni na mwenzake wa Kenya William Ruto, wamekutana na kujadiliana kuhusu azma ya kiongozi wa upinzani Kenya Raila Odinga ya kutaka kuwania uwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU).

Inaelezwa kuwa Odinga anatafuta uungwaji mkono kutoka mataifa tofauti ya Afrika ili kumsaidia kumrithi mwenyekiti wa sasa wa Tume ya AU Moussa Faki Mahamat wakati muhula wake utakapokamilika Februari 2025.

Majadiliano hayo yalijiri juzi baada ya Rais Museveni kuwakaribisha Rais Ruto na Odinga nyumbani kwake Kisozi.

"Ninamshukuru sana Rais Museveni kwa kuidhinisha kwa dhati kuteuliwa kwangu na kwa Rais Ruto kwa kuniunga mkono kikamilifu," Odinga aliandika kwenye X, zamani Twitter.

Aidha, inaelezwa kuwa mkutano wa viongozi hao watatu unaonekana kuwashangaza wengi katika nchi zote mbili, kutokana na yaliyojiri hivi karibuni kati ya mataifa hayo mawili, lakini pia kati ya Rais Ruto na Odinga. Mwaka jana.

Hivi karibuni Odinga aliongoza maandamano nchini Kenya dhidi ya serikali ya Rais Ruto wakiitupia lawama kuhusu gharama ya maisha, hali iliyozua mvutano wa kisiasa kati ya viongozi hao.

Hata hivyo, Novemba 2023 mzozo mkali kuhusu usambazaji wa mafuta ulizuka kati ya Kenya na Uganda isiyokuwa na bandari, huku Rais Museveni akisema nchi yake inadanganywa na vimelea na wafanyabiashara wa kati nchini Kenya.

Vile vile inaelezwa kuwa kutokana na mkutano huo Rais Ruto alishiriki kwenye X kwamba yeye na Rais Museveni wameafikiana kuhusu njia ya kusonga mbele, na kwamba maswala yanayoathiri usafirishaji wa bidhaa za petroli kati ya Kenya na Uganda yanatatuliwa. **BBC**

# TFF NA MATUMAINI KIBAO KWA SOKA LA UFUKWENI, TANZANITE

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limesema limeweka mazingira mazuri kwa timu mbili ikiwamo soka la ufukweni kwa wanaume na kikosi cha wanawake cha chini ya umri wa miaka 20 (Tanzanite), kwa ajili ya maandalizi ya All Afrika Games, 2023.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo, alisema tayari Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni chini ya Kocha wake, Boniface Pawasa, imeanza maandalizi kwa kufanya mazoezi wakitokea nyumbani kujiandaa na michuano hiyo.

Alisema mapema kuanzia sasa timu hiyo itaingia kambini na kikosi cha Wanawake U-20, kinatarajiwa kuingia kambini Machi 8, mwaka huu, chini ya Kocha wake, Bakari Shime.

"Kwa upande wetu mazingira ya kambi kwa hizo timu yanaenda vizuri na tunatarajia kuziona zinafanya vizuri katika michuano hiyo, ukiangalia tayari katika soka la wanawake Tanzania tumewajua wapinzani tutakaokutana nao," alisema Ndimbo.

Aliongeza kuwa wanaimani kubwa na timu zao kufanya vizuri katika michuano hiyo kwa sababu tayari timu ya soka la ufukweni imeanza mazoezi licha ya wachezaji kutokea nyumbani ila wataingia kambini muda wowote kuanzia sasa.

Kuhusu Tanzanite, alisema hawana presha juu ya timu hiyo ya wanawake kwa kuwa imekuwa na matokeo mazuri katika michuano mbalimbali na baadhi ya nyota wengi wana uzoefu kutokana na kupata nafasi ya kucheza katika timu ya Twiga Stars.

Tanzanite wamepangwa Kundi A, ikiwa na timu za Uganda, Ethiopia na wenyeji wa michuano hiyo, Ghana, itakayoanza kutimua vumbi Aprili mwaka huu.

## MWANA FA CUP...



Diwani wa Kata ya Bwembwera wilayani Muheza, Ally Nyangasa (kushoto), akikabidhi jezi na mpira mmoja kwa wachezaji wa timu ya Bwembwera FC juzi, baada ya kutinga ngazi ya Tarafa kuwania kucheza ngazi ya Wilaya katika michuano ya Mwana FA Cup iliyoshirikisha timu 35 kutoka kata 35. Kutoka kulia ni wachezaji wa timu hiyo, Charles Kapila, Isack Peter na Tuwa Gao. **PICHA. STEVEN WILLIAM**

# Ujenzi uwanja wa soka Arusha waanza

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

SERIKALI imeanza maandalizi ya kujenga uwanja wa mpira wa miguu jijini Arusha ikiwa ni maandalizi ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, ambayo yatafanyika nchini kwa ushirikiano wa Kenya na Uganda.

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, akizungumza jana jijini hapa katika kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara hiyo, alisema serikali inaendelea na ukarabati Uwanja wa Benjamin Mkapa, ujenzi wa viwanja vya kupumzikia Dodoma na Dar es Salaam.

Pamoja na hayo, amesema serikali imekamilisha mkakati wa taifa wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995.

Katika hatua nyingine, Msigwa alisema Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, anatarajiwa kufungua mkutano wa mwaka wa wadau wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa utakaofanyika jijini Dar es Salaam Februari 29, mwaka huu ambao utahudhuriwa na watu zaidi ya 800 kutoka taasisi zinazojishughulisha na utamaduni na sanaa, kifedha, Kampuni za Bima, makampuni ya simu, vyuo vya elimu kati na juu.

Aliyataja malengo ya mkutano huo kuwa ni kuwakutanisha wadau wa utamaduni kutoka sekta binafsi na umma waweze kujenga mtandao wa kufahamiana na kujadili kwa pamoja matatizo yanayoikabili sekta hiyo pamoja na kuwatambua na kuwatunuku waliofanya vizuri kwa kuwapatia zawadi.

# Maugo ajigamba kumpasua Mandoga

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Mada Maugo na Karim Mandonga, wanatarajiwa kumaliza ubishi wa nani zaidi kwenye pambano litakalofanyika mapema Aprili mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Mabondia hao watapanda ulingoni kwenye pambano la raundi 6 na kilo 79.

Akizungumza na Nipashe jana, Maugo alisema anataka kutoa burudani kwa mashabiki wake baada ya kukaa muda mrefu bila kupigana, kwani anaamini Mandonga hamuwezi.

"Nitamfundisha adabu Mandonga katika pambano hilo, hajawahi kupigwa alikuwa anaguswa guswa kwenye mapambano aliyocheza, nitampasua ili ajue mimi ni nani," alisema Maugo.

Bondia huyo alisema anasubiri tarehe ya pambano hilo mara baada ya kukamilika kwa mazungumzo ya waandaaji pamoja na wadhamini.

Kocha wa Maugo, Mmarekani Seko Tongola, alisema amekuja hapa nchini kwa ajili ya kumsimamia bondia wake huyo.

"Kesho (leo), nitaanza kumpa mbinu bondia wangu zitakazomsaidia kufanya vizuri kwenye pambano hilo kwa kuwa hajapigana muda mrefu, ninapaswa kumpa mazoezi ya nguvu ili aimarishe mwili wake kabla ya kukutana na mpinzani wake," alisema Tongola.

Alisema kabla hajawasili alikuwa anamfundisha kwa njia ya video akiwa nchini Marekani, lengo likiwa ni kuhakikisha ushindi unapatikana.

Alisema anamfahamu Mandonga amek



## ZISIKUPITE

### DAVIES ANUKIA MADRID

REAL Madrid imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 23, na watatarajia kukamilisha dili hilo msimu huu wa majira ya joto au 2025, atakapokuwa mchezaji huru. **(Athletic)**

### POCHETTINO HAKIELEWEKI

MUSTAKABALI wa Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, haujulikani baada ya timu yake kupoteza mchezo wa fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Liverpool, huku Kocha wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim, akitarajiwa kuchukua nafasi yake. **(Mail)**

### MAN UNITED KUUZA KUMI

MANCHESTER United inatarajiwa kuwatoa wachezaji kadhaa msimu huu huku winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, akiwa miongoni mwa wale ambao watakuwa tayari kuwauza. **(Mail)**

### CHELSEA KUMUUZA CHOLOBAH

CHELSEA inatumaini kumuuza mlinzi wake, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24, na mshambuliaji wa Albania, Armando Broja, huku mustakabali wa Kiungo wa England, Conor Gallagher(24), na beki wa Hispania, Marc Cucurella mwenye miaka 25, ukiwa shakani. **(Telegraph)**

### PALHINHA AGOMBEWA

KLABU za Bayern Munich, Liverpool na Arsenal zipo kwenye mbio za kumnunua kiungo wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28, msimu huu wa majira ya joto. **(Football Insider)**

### DE BRUYNE AITAKA MLS

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Kevin de Bruyne, angependelea kuhamia Ligi Kuu ya Marekani (MLS), badala ya Ligi Kuu ya Saudi Pro. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ubelgiji anatimiza miaka 33, msimu huu wa majira ya joto, wakati mkataba wake unaingia mwaka wake wa mwisho. **(Athletic)**

### ZIDANE AHUSISHWA JUVE

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 51, yuko tayari kufundisha nchini Italia, huku nyota huyo wa Ufaransa akihusishwa na kurejea Juventus. **(La Gazzetta dello Sport)**

### RAMSDALE KUONDOKA

GOLIKIPA wa England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25, ana nia ya kuondoka Arsenal msimu wa majira ya joto baada ya kupoteza nafasi yake kwa kipa wa Hispania, David Raya, 28. **(Football Insider)**

### PHILOGENE AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika harakati za kumsaka mshambuliaji wa Hull City, Jaden Philogene mwenye umri wa miaka 22, ingawa Aston Villa wana kipengele cha kumnunua winga huyo. **(Teamtalk)**

### FORSON KUONDOKA UNITED

MCHEZAJI wa Kimataifa wa England, Omari Forson mwenye umri wa miaka 19, anaweza kuondoka Manchester United msimu huu wa majira ya joto, huku kiungo huyo mshambuliaji akimaliza mkataba wake Old Trafford. **(Athletic)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PSG SASA TUJIFUNZE KUISHI BILA MBAPPE - ENRIQUE

●●● Ninapotaka kumchezesha, nitafanya, nisipomchezesha, hatacheza...

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, amekiri timu yake inahitaji kujiandaa kwa kuondoka kwa Kylian Mbappe msimu huu wa majira ya joto baada ya kumtoa nahodha huyo wa Ufaransa wakati wa sare na Rennes, Jumapili.

Mbappe alitolewa dakika ya 65 na PSG wakiwa nyuma kwa bao 1-0 nyumbani kwa Rennes na nafasi yake kuchukuliwa na Goncalo Ramos, aliyefunga bao la penalti la kusawazisha dakika ya 97.

„Ni rahisi sana: Hivi karibuni au baadaye, inapotokea, lazima tuzoee kucheza bila Kylian," alisema Enrique alipoulizwa kuhusu uamuzi huo baada ya mchezo huo.

„Ninapotaka kumchezesha, nitafanya, nisipomchezesha, hatacheza."

ESPN iliripoti mapema mwezi huu kwamba Mbappe aliiarifu PSG kuhusu nia yake ya kuondoka wakati mkataba wake utakapomalizika msimu huu wa majira ya joto, na bado yuko kwenye mazungumzo na Real Madrid, ambao wana matumaini ya kumpata mshambuliaji huyo.

Hii ni mara ya kwanza kwa kocha huyo kuzungumzia kuondoka kwa Mbappe katika klabu hiyo ya Ligue 1 ambako amekaa kwa miaka sita iliyopita.

Katika mkutano na waandishi wa habari Februari 16, mwaka huu, Luis Enrique alisema: „Nitajaribu kumaliza mada hii. Sina maoni yoyote ya kutoa.

„Pande zinazohusika bado hazijasema chochote hadharani, Kylian Mbappe hajasema chochote hadharani.

„Wakati pande zote mbili zitakapozungumza, nitatoa maoni yangu."

Mbappe amefunga mabao 21 katika mechi 21 za Ligue 1 msimu huu, pamoja na mabao manne katika mechi saba za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

PSG itakabiliana na Monaco Ijumaa hii kabla ya mechi ya mkondo wa pili ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Sociedad Machi 5, mwaka huu ambapo tayari wanafaida ya kuongoza kwa mabao 2-0.

# MADRID WAKARIBIA KUMTWAA DAVIES

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wamefikia makubaliano ya mdomo na Alphonso Davies kuhusu kumsajili nyota huyo kutoka Bayern Munich mwaka 2024 au 2025, kwa mujibu wa The Athletic.

'Los Blancos' hao wamekuwa wakimwania Davies kwa muda mrefu wa msimu hadi sasa na wanamwona kama mmoja wa walengwa wao wa kipaumbele cha uhamisho pamoja na Kylian Mbappe wa PSG.

Mkataba wa raia huyo wa Canada pale Allianz Arena unaendelea hadi msimu wa majira ya joto wa 2025, lakini mazungumzo bado hayajafanikiwa juu ya mkataba mpya.

Ripoti kutoka Ujerumani wiki iliyopita zilieleza Bayern walikuwa wakikubali zaidi kwamba wanaweza kuhitaji kumuuza Davies katika dirisha la majira ya joto 2024 ili kurudisha ada na kuzuia kumpoteza bila malipo mwaka mmoja baadaye.

Sasa, The Athletic limeripoti kwamba Madrid wamekubaliana na Davies kwamba atasajiliwa ndani ya madirisha mawili yajayo ya joto.

Juhudi za Madrid zimeongozwa na skauti mkuu, Juni Calafat na Mkurugenzi Mkuu, Jose Angel Sanchez, ambao wamemtaka Davies kutoongeza mkataba wake Bayern ili kufanya mchakato wa uhamisho kuwa mwepesi.




Davies pia anatakiwa na klabu za Ligi Kuu England na pia kumekuwa na 'maslahi ya awali' kutoka kwa Barcelona, lakini hatimaye anachopendelea ni kujiunga na Madrid.

Bayern hawajafanya mazungumzo na Madrid kuhusu Davies na bado wangependelea kusaini mkataba mpya, lakini watatafuta kumuuza ikiwa hakuna mafanikio katika mazungumzo yaliyofikiwa kufikia majira ya joto.

Hali hiyo imefananishwa na Madrid kumnasa Toni Kroos kutoka 'Bavaria' mwaka 2014, huku kiungo huyo akielekea Santiago Bernabeu kwa punguzo la bei kutokana na hali ya mkataba wake.

Davies ameichezea Bayern mechi 180 tangu alipojiunga nayo mwaka 2018 akitokea Vancouver Whitecaps ya Ligi Kuu ya Marekani (MLS), na hivyo kuimarisha hadhi yake ya kuwa mmoja wa mabeki bora zaidi wa kushoto duniani.

## Antony sasa kuuzwa United

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United wanatarajiwa kusikiliza ofa kwa ajili ya kumuuza Antony wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto, kwa mujibu wa ripoti.

Antony ameshindwa kung'ara pale United tangu kuhamia hapo Old Trafford kutoka Ajax kwa pauni milioni 82 katika msimu wa majira ya joto wa 2022.

Ingawa kulikuwa na nyakati nzuri wakati wa kampeni ya kwanza ya Mbrazil huyo - ikiwa ni pamoja na ushindi mzuri dhidi ya Barcelona kwenye Ligi ya Europa - ameshindwa kufunga msimu huu, akikosa kusajili bao au kusaidia katika mechi 20 za Ligi Kuu England.

Nje ya uwanja, Antony pia amekabiliwa na shutuma huku kukiwa na uchunguzi huko Manchester na Sao Paulo kwa kumpiga mpenzi wake wa zamani.

Gazeti la Manchester Evening News limeripoti kuwa kama sehemu ya mipango ya wadau wapya wa INEOS ya kuuza wachezaji ili kupunguza hofu juu ya kutimiza Kanuni za Faida na Uendelevu za Ligi Kuu, klabu hiyo inatarajiwa kupokea ofa kwa Antony msimu huu wa majira ya joto.

Pia, wapo walioko kwa mkopo Jadon Sancho, Donny van de Beek na Hannibal Mejbri, huku Anthony Martial na Tom Heaton wakitarajiwa kuachwa hadi mikataba yao itakapomalizika msimu huu wa majira ya joto.

Casemiro amekuwa akivutiwa na Ligi Kuu ya Saudia, 90min ilifichua wiki iliyopita Al Ittihad na Al Nassr zinatayarisha ofa za kumnunua Raphael Varane.

Ripoti hiyo pia imewataja Aaron Wan-Bissaka, Victor Lindelof na Facundo Pellistri kama mali zinazoweza kuuzwa kutokana na mikataba yao kumalizika 2025.

United wanaonekana kutokusudia kuchukua kipengele cha ununuzi katika makubaliano yao ya mkopo na Fiorentina kwa Sofyan Amrabat na atarejea Florence mwishoni mwa msimu.

Mustakabali wa Marcus Rashford pia haujulikani kufuatia kushuka kwa kiwango cha kutisha msimu huu - 90min inaelewa kuwa yumo kwenye orodha fupi ya PSG ya mbadala wa Kylian Mbappe - wakati Sir Jim Ratcliffe amefichua kuwa klabu itaangalia tena hali ya Mason Greenwood kutoka mkopo wake kule Getafe.

United wana matumaini ya kuuza wachezaji wasiopungua kumi wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto.



## Grealish mambo magumu Man

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema Jack Grealish, atarejea kwenye kikosi chake na kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara wakati kiwango chake kitakapoimarika.

Kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 28, alianza mechi 41 akiwa na City katika kampeni ya kushinda mataji matatu msimu uliopita, ikijumuisha fainali za Kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ameanza mechi 19 pekee msimu huu, zikiwamo saba za Ligi Kuu England.

"Ni mchezaji yule yule, ana kocha yule yule, na jinsi tunavyocheza haijabadilika," alisema Guardiola.

"Ni jinsi tu amefanya. Hiyo ndiyo tofauti."

Msimu huu, Grealish amekuwa na dakika chache katika Ligi Kuu na kati ya mechi 19 alizoanza, nne alicheza kwenye Ngao ya Jamii, Kombe la Super Cup na mechi zote mbili Kombe la Klabu Bingwa Dunia nchini Saudi Arabia.

**Mara ya mwisho alianza mchezo wa ligi Desemba 30 , mwaka jana dhidi ya Sheffield United , ambapo nafasi yake ilichukuliwa na chipukizi Oscar Bobb baada ya dakika 52.**

Mchezaji huyo aliyenunuliwa kwa pauni milioni 100 alibaki kwenye benchi wakati wote wa ushindi dhidi ya Bournemouth Jumamosi na hakuna uhakika kwamba ataanza mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA huko Luton. "Nilisema tangu siku ya kwanza, tunamhitaji," alisema Guardiola.

"Ana ubora maalum kwa timu yetu. Lakini inategemea na yeye mwenyewe. Ninatumaini anaweza kufanya vema."

Grealish si mchezaji wa kwanza kujikuta ndani na nje ya kikosi cha Guardiola, hayo ni matakwa ambayo kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich ameweka kwa wachezaji wake.

Na mchezaji huyo wa Kimataifa wa England ameonywa kuwa hatapewa muda wa kujirekebisha kurejea City.

"Siwezi kuwapa wachezaji mechi tatu au nne ili kupata mdundo wao," aliongeza Guardiola. "Lazima watafute mdundo wa kucheza kwa dakika 20 au 90.

"Katika kiwango cha juu, timu haisubiri kuwa fiti. Huwezi kumpa mtu michezo mitatu au minne ili awe fiti, vipi wale 10 ambao hawachezi wanastahili kutocheza?

"Lazima uone vipindi vya mazoezi na maelezo yote. Wachezaji wanapaswa kujiridhisha kuwa wanastahili kucheza."

HABARI MICHEZO

# AZAM FC SASA YAKIRI UBINGWA LIGI KUU BASI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons, Azam FC imetangaza rasmi kunyoosha mikono juu kwa kuachia ngazi kwenye vita vya kuwania taji la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na sasa imeamua kuandaa timu kwa ajili ya msimu ujao.

Azam FC wako nafasi ya pili na alama 37 wakicheza michezo 17, wakati Simba yenye pointi 36 katika nafasi ya tatu, ina michezo miwili mkononi na Yanga ikiongoza msimamo wa ligi hiyo kwa pointi 43 ikicheza mechi 16.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, alisema hakuridhishwa na matokeo hayo, hivyo wanapaswa kuwa makini na si kuhamaki kwa sababu ni mpira huwa una matokeo ya kushangaza.

Alisema kwa sasa wanapigania kutafuta matokeo kila mechi ili kujiweka sawa katika kufikia malengo yao huku wakiendelea kujenga timu yao kwa ajili ya kushindania ubingwa kwa msimu ujao.

"Tunakuwa na wakati mgumu, kwa sababu washambuliaji wetu hawachezi kwa ubora wao, sitaki kutaja majina, lakini tukiangalia michezo tofauti tunaweza kuona ubora wao.

"Hivyo kazi yetu ni kuwasaidia kuwarudisha viwango vyao kwani hawajapoteza ubora, lakini kiutimamu wa mwili, kiakili wanatakiwa kurudishwa ubora wao huo. Lakini ndio mpira tunaweza kuwa na mishangao mingi kwenye soka chochote kinaweza kutokea, kama maisha unachotakiwa ni kuangalia mbele," alisema Dabo.

Aliongeza kubwa ni kujiamini na kuamini kazi yako ili kubaki katika njia sahihi ya kupata ufumbuzi na utatuzi, lakini hawapaswi kuhamaki na kukata tamaa katika kupigania mipango yao ya kusaka nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

# Tabora United yaapa kuzindukia Prisons leo

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Tabora United ambayo haijapata ushindi tangu kuingia kwa mwaka mpya 2024, leo itakuwa ugenini, Uwanja wa Sokoine Mbeya kucheza dhidi ya Prisons katika mechi ya raundi ya 18 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku ikiwaahidi kuwafuta machozi mashabiki wake.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala, alisema jana licha ya kuwa na matokeo yasiyoridhisha, lakini wamejipanga vema kuhakikisha wanapata ushindi wa kwanza leo tangu kuanza kwa mwaka huu.

"Tumejipanga, tunajua mechi za ugenini zinakuwa na changamoto kwa maana ya upatikanaji wa matokeo, tuna uhitaji mkubwa sana na kushinda kupata pointi tatu kwa sababu ukizingatia hatupo vizuri kwenye msimamo wa ligi na hili ni duru la lala salama, hii itakuwa ni mechi yetu ya tatu kwenye mzunguko huu wa pili kwa hiyo hakuna kingine tunahitaji pointi tatu tu ili kuwafuta machozi mashabiki wetu na tuna uhakika leo tutazindukia kwao," alisema Mwagala.

Mara ya mwisho kwa Tabora United kushinda ilikuwa ni Desemba Mosi mwaka jana ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, lakini baada ya hapo ikacheza mechi saba bila kupata ushindi.

Desemba 5 ilitoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Mashujaa, Desemba 8 ikachapwa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Ihefu, kabla ya kudunguliwa bao 1-0 na Yanga, Desemba 23 Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, ikiwa ni mechi ya mwisho kwa mwaka jana.

Mwaka huu ilikutana na kipigo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Simba, sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo ikichezwa nyumbani Februari 11, suluhu dhidi ya Azam FC Februari 10 na sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Fountain Gate, Jumapili iliyopita.

Ina pointi 18 kwa michezo 17 iliyochezwa, ikiwa nafasi ya 12, na inacheza dhidi ya Prisons iliyo nafasi ya saba na pointi zake 21.

Mechi zingine zitakazopigwa leo kwenye Uwanja wa Liti Singida Ihefu FC itakapoikaribisha Mashujaa FC, Singida Fountain Gate itakuwa CCM Kirumba kukipiga dhidi ya Azam FC, na Geita Gold itakuwa Uwanja wa Nyankumbu, Geita kuisubiri Kagera Sugar.

**SAFARI IMEANZA...**




Winga wa Yanga, Augustine Okrah, akielekea Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana tayari kwa safari ya kuelekea Misri kwenye mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayopigwa Uwanja wa Cairo Ijumaa wiki hii. **PICHA: YANGA**

## GAMONDI: HAIJAISHA

INATOKA UK. 24

huo kusaka ushindi licha ya kutambua ubora wa wapinzani wao hao.

"Kila mmoja anapenda kuona wachezaji wanapata matokeo na uzuri ni kwamba wanajituma na kutimiza majukumu yao kwenye mechi ambazo tunacheza na kutaka matokeo.

"Ni furaha tumefuzu kucheza robo fainali ambayo tulikuwa tunaitafuta kwa miaka mingi, lakini bado tuna kazi kubwa ya kufanya katika mchezo wetu wa mwisho dhidi ya Al Ahly," alisema Gamondi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema timu imeondoka jana saa 11:55 jioni kuelekea Misri kwa Shirika la Ndege la Ethiopia ambapo walitarajia kufika Ethiopia saa 2:33 usiku na kisha kuwasili Misri saa saba usiku.

"Tunaenda na msafara wa watu 60 na ambao umegawanyika katika makundi matatu; wachezaji 24, benchi la ufundi 13 na watendaji wakuu na maofisa wa klabu 23. Tunatambua ni mchezo muhimu na wenye ushindani mkubwa kulingana na ubora wa mpinzani wetu, hivyo tumejiandaa vizuri," alisema Kamwe.

## Simba SC kula kiporo TRA leo

INATOKA UK. 24

kushinda mechi hii ili tuwe kwenye njia ya kuchukua Kombe la FA, pamoja na kuwafurahisha mashabiki wetu," alisema Banchikha.

Wakati huo huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema mchezo wa Jumamosi si tu kwamba utakuwa ni wa kusaka ushindi ili kwenda hatua ya robo fainali, bali ni wa kulipiza kisasi cha kufungwa na timu hiyo, Oktoba 24, 2021 kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa.

"Sidhani kama kuna Mwanasimba amesahau machungu ambayo tumewahi kuyapitia na niwaibie siri, Rais wa Heshima wa Klabu, Mohamed ‚Mo' Dewji, aliugua wiki mbili kutokana na maumivu tuliyoyapata ambayo tulisababishiwa na Jwaneng Galaxy, nadhani sasa muda umefika wa kwenda kufuta haya maumivu. Tunakwenda kulipa kisasi, ni muda wetu sasa na mchezo huu tumeupa jina la ‚Vita ya Kisasi'," alisema Ahmed.

Alisema katika mechi hiyo wanahitaji vitu viwili, kutinga robo fainali na kulipa kisasi kitu ambacho kimewafanya kwa sasa kuwa kwenye maandalizi makali kwa ajili ya mchezo huo.

Simba ilichapwa mabao 3-1 kwenye mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kushindwa kuingia makundi kwa tofauti ya mabao ya nyumbani na ugenini baada ya matokeo ya jumla kuwa 3-3.

Na hii ni baada ya Simba kushinda mabao 2-0 katika mechi ya kwanza ugenini, Oktoba 17, 2021, Jwaneng Galaxy ikasonga mbele kwa kufunga mabao mengi ugenini, Wekundu wa Msimbazi wakashindwa kutinga makundi na kwenda Kombe la Shirikisho ambalo huko walifikia hatua ya robo fainali.

# Michezo

Jumatano Februari 28, 2024
Nipashe


PSG sasa tujifunze kuishi bila Mbappe - Enrique UKURASA 21



# GAMONDI: HAIJAISHA MPAKA AL AHLY AKAE

## ●●●Waifuata na msafara wa watu 60, asema ni kazi ngumu, lakini wamejipanga kwa...

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kukata tiketi ya kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku ikiwa na mechi moja mkononi, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hawezi kusema ameridhika kwa kuwa kazi haijaisha hadi lengo lao litimie kwenye michuano hiyo ya kimataifa ikiwa ni pamoja na ushindi dhidi ya Al Ahly.

Wiki iliyopita Yanga ilikata tiketi hiyo baada ya kuifunga CR Belouizdad mabao 4-0, hivyo kuungana na Al Ahly ya Misri kuwa timu zilizofuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi D.

Hata hivyo, Al Ahly na Yanga zitakutana Ijumaa wiki hii nchini Misri kuhitimisha mechi zao za hatua ya makundi, lakini pia mchezo huo ndio utakaoamua timu itakayoongoza kundi lao.

Yanga yenye pointi nane inahitaji ushindi ili kuongoza kundi hilo, wakati Al Ahly ambayo ipo kileleni ikiwa na alama tisa, yenyewe ikihitaji sare yoyote ama ushindi ili kuhitimisha hapo ilipo.

Kikosi cha Yanga kimeondoka jana jioni kuelekea nchini Misri kwenye mchezo wao huo wa mwisho katika hatua ya makundi kikiwa na matarajio makubwa ya kupata ushindi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Gamondi alisema anaifahamu vizuri Al Ahly na ana kazi kubwa ya kupata ushindi katika mchezo huo ili kuongeza hali ya kujiamini.

Alisema kila mchezaji yupo tayari kuona wanaendelea kuwa kwenye ubora na wanakwenda katika mchezo

INAENDELEA UK. 23



Gamondi

# Simba kula kiporo TRA leo

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba leo kitashuka kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, saa 1:00 usiku, kumalizia mechi yake ya kiporo ya Kombe la FA dhidi ya TRA kutoka Kilimanjaro, huku Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, akisema itakuwa maalum kwa ajili ya kuangalia marekebisho aliyoyafanya kabla ya kuivaa Jwaneng Galaxy ya Botswana Jumamosi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyopewa jina la ‚Vita ya Kisasi.'

Mechi itakayochezwa leo, awali ilipigwa kalenda kutokana na Simba kusafiri kwenda nchini Ivory Coast kukabiliana na Asec Mimosas katika mechi ya raundi ya tano ya Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa Uwanja wa Felix Houphouet Boigny jijini Abdijan Ijumaa iliyopita na kumalizika kwa suluhu.

Mchezo huo utakamilisha mechi ya 16 kati ya timu 32 zilizotakiwa kucheza hatua hiyo ya raundi ya tatu ya kombe hilo ili kusaka bingwa atakayeiwakilisha



Benchikha

Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika msimu ujao.

Tayari jumla ya mechi 15 zimeshachezwa na mechi ya leo itakamilisha idadi ya michezo 16, kabla ya kupangwa kwa ratiba nyingine kwa ajili ya michezo ya kwenda robo fainali.

Kocha Mkuu wa Simba, Benchikha, amesema mechi ya leo ina umuhimu kwake mara mbili kwa sababu inamwezesha kuchezesha wachezaji wengi ambao atawatazama na kuangalia kama wanaweza kumpa kitu Jumamosi katika mechi muhimu ya Ligi ya Mabingwa, lakini kuangalia kile ambacho amekifundisha na kukirekebisha uwanja wa mazoezi baada ya mechi iliyopita.

"Kulikuwa na mapungufu kadhaa katika mechi iliyopita hasa ya kutumia nafasi, tumelifanyia kazi mazoezini, nataka niangalia leo kama limepungua kwa kiasi gani, hiyo ni moja, lakini nitawatumia baadhi ya wachezaji ili niwaangalie kama wanaweza kunipa angalau kitu katika mechi ya Jumamosi na pamoja na yote tunahitaji

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042